epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710 LIKE & FOLLOW US
Jumatatu Desemba 2, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581878
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

ZITTO ASEMA...

# Tunawajua waliomteka Abdul Nondo, wamwachie



• **Adaiwa** kutekwa alfajiri kwenye Stendi ya Magufuli; polisi walonga...*Endelea ukurasa 3*



UKURASA WA 12
**WACHEZAJI WAWILI MAPATINA BORA ZAIDI WA SOKA DIMBANI**

UKURASA WA 3
**Risiti** feki za EFD miradi taasisi za serikali zashtua



UKURASA WA 19
**Mahakama** ya Mafisadi yamtia hatiani, yataifisha gari la kifahari



UKURASA WA 19
**Trump** sasa atishia nchi zinazounga mkono China, Russia



UKURASA 2

Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na viongozi mbalimbali wa serikali pamoja na wa kimila wa jamii ya Kimaasai 'Malaigwanani' wanaoishi Ngorongoro na maeneo jirani katika Ikulu ndogo ya Arusha jana. **PICHA: IKULU**

SIKU YA UKIMWI

## Serikali yaorodhesha vigingi kutokomeza UKIMWI Bara, Zanzibar

UKURASA 2

# Samia kuunda tume mbili kuchunguza Ngorongoro

**MICHEZO** **RAMOVIC AKOSHWA KIWANGO CHAMA** UK.24

**KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Serikali yaorodhesha vigingi kutokomeza UKIMWI nchini

**Na Halfani Chusi**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango ameelekeza Tume ya Kudhibiti UKIMWI nchini (TACAIDS) kwa kushirikiana na wizara za kisekta, wadau na jamii kwa ujumla kuweka mkazo katika kudhibiti mazingira yanayochochea maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU).

Alielekeza hayo jana wakati wa maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani yaliyofanyika Kitaifa kwenye Uwanja wa Majimaji, mjini Songea, mkoani Ruvuma.

Alitaja vigingi vilivyopo katika kutokomeza UKIMWI nchini vinajumuisha jamii kuwa na mtazamo hasi dhidi ya walioambukizwa virusi hivyo, hata kuchangia kurudisha nyuma jitihada za kupambana na UKIMWI.

Alisema mtazamo hasi huwafanya wahitaji kushindwa kupata huduma kwa kuonekana kuwa hawastahili na hivyo kutengwa. Alionya kuwa unyanyapaa husababisha woga unaoathiri upimaji kwa hiari na upatikanaji huduma nyingine kama za unasihi pamoja na ARV kwa wale wanaoishi na VVU.

Aliwataka vijana kujitambua, kujithamini na kutunza maisha yao kwa kujikinga na maambukizi mapya ya VVU kwa kuwa kasi ya maambukizi katika kundi hilo inaonekana kuwa kubwa. Takwimu za hali ya UKIMWI nchini zinaonesha kundi la vijana ndo hasa wa kike liko katika hatari zaidi ya kupata maambukizi mapya ya VVU.

Makamu wa Rais aliwataka wananchi kuzingatia maudhui ya elimu inayotolewa kupitia kampeni mbalimbali kwa ajili ya kubadili tabia, kuachana na mila zinazoweza kuwa vichocheo vya maambukizi na kuendelea kujikinga na maambukizi mapya ya VVU.

Alisema hali ya maambukizi mapya inaonekana kuchochewa zaidi na mazingira na tabia hatarishi hususan ulevi uliopindukia, ngono zembe, kuwa na wapenzi wengi na matumizi ya dawa za kulevya.

Alisema mapambano dhidi ya UKIMWI yaliyoanza takriban miongo minne iliyopita, yamepata mafanikio. Matokeo ya utafiti wa viashiria vya VVU na UKIMWI uliofanyika mwaka 2022/23, yanaonesha maambukizi mapya mionngoni mwa watu wazima wenye umri kuanzia miaka 15 ni watu 60,000 kwa mwaka. Kiwango cha ushamiri wa VVU kitaifa ni asilimia 4.4 ambapo jumla ya watu 1,548,000 wanaishi na VVU.

"Kiwango cha ushamiri wa VVU kwa wenye umri kuanzia miaka 15 na zaidi kwa upande wa Tanzania Bara ni asilimia 4.5 na asilimia 0.4 kwa upande wa Zanzibar. Viwango vya ushamiri kwa mikoa ya Tanzania Bara vinaanzia asilimia 1.7 (Kigoma) hadi asilimia 12.7 (Njombe). Mikoa mitatu ya Mbeya, Iringa na Njombe ina viwango vya ushamiri zaidi ya asilimia tisa (9) ambayo ni mara mbili ya kiwango cha kitaifa," alisema.

Awali Waziri wa Afya, Jenista Mhagama alisema wizara itaendelea kufanya maboresho ya kuhakikisha uamuzi wa kuunganisha mwitikio kwa kujumlisha uratibu wa magonjwa ya ngono, homa ya ini na UKIMWI kama vihatarishi vinavyofanana na vinavyofananishwa katika njia za maambukizi, kwa pamoja vinawekewa mkakati madhubuti wa kupambana navyo ili kuimarisha afya za watanzania.

**ZANZIBAR**

Akiwa mkoa wa Kusini Pemba jana, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, alisema changamoto zinazohusiana na haki za binadamu katika upatikanaji huduma za UKIMWI zinachangia kwa kiasi kikubwa kuzorotesha juhudi za serikali na ulimwengu kwa ujumla katika kumaliza tatizo la UKIMWI.

Alisema changamoto hizo, ukiwamo unyanyapaa na watu kulazimishwa kupima, na unyanyasaji wa kijinsia hupelekea watu kukosa na kuogopa kuzifikia huduma za kujikinga na VVU pamoja na za matibabu kwa wanaoishi na VVU.

Makamu wa Rais alisema hofu ya unyanyapaa inasababisha watu waogope kwenda vituo vya afya kuchunguza afya zao na ni miongoni mwa yanayosababisha wanaoishi na VVU kushindwa kutumia dawa ipasavyo.

Othman pia alikosoa tabia ya baadhi ya mashirika na taasisi kuwalazimisha wafanyakazi wao hasa inapotokea haja ya kuongezwa mikataba, kupimwa kwa lazima, jambo ambalo ni kinyume cha sheria za afya Zanzibar.

"Mbaya zaidi ni katika baadhi ya vituo vya afya hapa Zanzibar kuwalamisha wananchi kupima VVU kabla ya kupatiwa huduma muhimu za afya wanazozihitaji, ukiwamo upasuaji licha kwamba kisheria uchunguzi huo unatakiwa kuwa wa hiari," alisema.

Alionya kuwa hali hiyo inaweza kuchochea maambukizo mapya katika jamii kwa kuwa watu wenye wasiwasi wa kuishi na VVU hulazimika kuzikimbia huduma ambazo ni muhimu katika kuimarisha afya zao na kusaidia kupunguza maambukizo kwa watu wanaowazunguka na jamii kwa jumla.

Hata hivyo, Makamu wa Rais alisema Zanzibar haina budi kujipongeza kwa mafanikio ya kudibiti kiwango cha maambukizo ya VVU kubaki chini ya asilimia moja na kwamba utafiti wa karibuni unaonesha kwamba ni asilimia 0.4 ya wakazi wa Zanzibar wanaoishi na VVU.

Alisema hatua hiyo pia imesaidia kupunguza vifo vinavyotokana na maradhi ya UKIMWI Zanzibar kutoka 519 mwaka 2020 hadi watu 362 mwaka 2023 na kupunguza idadi ya maambukizo mapya kutoka watu 274 mwaka 2020 hadi maambukizo 190 kwa mwaka 2023.

Othman alisema kuwa ifikapo mwaka 2025, Zanzibar inatarajia kuungana na ulimwengu kufikia shabaha ya 95 tatu, hata kumaliza kabisa tatizo la UKIMWI ifikapo mwaka 2030.

Alisema matumaini hayo yanatokana na kwamba hadi kufikia mwaka 2024, shabaha ya 95 ya kwanza ya kujitambua tayari imefikiwa kwani aslimia 90 ya wanaokisiwa kuishi na VVU wanajitambua na 95 ya pili ni kwamba hadi kufikia Septemba 2024 asilimia 98 ya wanaojitambua wanaendelea kutumia dawa na ile 95 ya tatu ni kwamba asilimia 95 ya wanaotumia dawa, wameweza kupunguza makali ya virusi.

Makamu wa Rais alisema mafanikio hayo yametokana na ushirikiano ya serikali na wadau na maendeleo, akiwashukuru wadau hao kutokana na ushirikiano wao pamoja na misaada ya kiufundi na fedha wanazotoa katika kupambana na tatizo la UKIMWI nchini.

Hata hivyo, alielekeza kuongeza nguvu katika kukabili ipasavyo mazingira hatarishi yanayoweza kuchangia maambukizo mapya na kwamba ni wajibu wa kila mmoja kuishi kwa tahadhari ya kujilinda dhidi ya VVU. Alihimiza jamii kushikamana na kuwa na utaratibu bora wa maelezi ili watoto na vijana wasitumbukie katika vishawishi.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Harous Said Suleiman alisema shughuli mbalimbali za kutoa elimu na kuhamasisha watu kupima kujua hali yao zilifanyika kwa ufanisi mkubwa kuelekea maadhimisho hayo.

Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mapambano dhidi ya UKIMWI (UNAIDS), Dk. Gorge Loy alisema bado zipo changamoto kwa watu walio na VVU kufikiwa na huduma, huku unyanyapaa dhidi yao ukiendelea katika jamii.

Mwenyekiti wa Tume ya Ukimwi Zanzibar, Dk . Ali Salim alisema kuwa katika kufikia malengo ya mapambano hayo, kuna haja kuangaliwa na kubadilishwa sheria zinazosimamia maradhi ya UKIMWI kutokana na suala la unyanyapaa na ubaguzi kuendelea ndani ya jamii dhidi ya watu wanaoishi na VVU.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.***



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akihutubia wakati wa Maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani, yaliyofanyika Kitaifa katika Uwanja wa Majimaji, Songea, mkoani Ruvuma jana.
**PICHA: OMR**


IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO DISTRICT AT MOROGORO
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.28732 OF 2024
IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE SEBASTIAN NYAMBAYA MIYAGA—–DECEASED
AND
IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTER OF ADMINISTRATION BY

1. PHILOMENA THEOPHIL SEBASTIAN—–PETITIONER
2.............................................

GENERAL CITATION
(Under Rule 75 of Probate Rules and any other enabling Provision of the Law)

ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above- named pepetitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 03 day of DECEMBER, 2024.
Dated at Morogoro this ———-day of NOVEMBER,2024.

..................................
PRINCIPAL/SENIOR/RESIDENT MAGISTRATE
MOROGORO DISTRICT COURT


# Samia kuunda tume mbili kuchunguza Ngorongoro

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema atatunda tume mbili kuchunguza kinachojiri Ngorongoro, hata kusababisha kuwapo malalamiko kwa wakazi wa eneo hilo.

Amesema tume moja itachunguza na kutoa mapendekezo kuhusu masuala ya ardhi yanayolalamikiwa na wakazi wa Ngorongoro na nyingine itaangalia utekelezaji zoezi zima la uhamiaji kwa hiari kutoka eneo la Hifadhi ya Ngorongoro.

Rais Samia aliyasema hayo jana katika Ikulu Ndogo ya Arusha wakati akizungumza na viongozi wa kimila wa jamii ya Kimaasai (Malaigwanani) wanaoishi Ngorogoro.

Taarifa iliyotolewa kwa umma na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais-Ikulu jana, ilieleza kuwa mkutano huo ulifanyika kwa lengo la kuwasikiliza viongozi hao kufuatia kuwapo malalamiko dhidi ya baadhi ya uamuzi wa serikali unaohusu eneo la Ngorongoro.

Rais Samia aliwahakikishia serikali itaendelea kuimarisha utendaji kazi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) kwa lengo la kuimarisha uhusiano kati ya serikali na jamii hiyo.

Vilevile, alisisitiza ulazima wa wananchi kushirikishwa ipasavyo katika upangaji na utekelezaji miradi inayopita kwenye maeneo yao.

Rais Samia alisisitiza Tanzania ni nchi inayojivunia umoja wa kitaifa na yenye serikali inayowahudumia Watanzania wote. Hivyo, akaitaka Ofisi ya Rais - TAMISEMI kushughulikia changamoto zinazojitokeza ikiwamo kukosekana baadhi ya huduma za msingi za kijamii katika eneo la Ngorongoro.

**THRDC, LHRC**

"Tunapongeza kwa hatua ya kukutana na watu wa Ngorongoro, imekuwa ni kilio cha muda mrefu, tumesisitiza akaonane na watu wake, huenda angekutana nao mapema zaidi yaliyotokea yasingetokea hivyo, ila tunashukuru angalau amekutana nao," alisema Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), Onesmo Olengurumwa.

Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (THRDC), Dk. Anna Henga, alisema kuunda tume si kitu cha kushangiliwa sana, bali ni matokeo ya tume kuwa wazi na kufanyiwa kazi. Alitahadharisha kuwa tume nyingi zinaundwa na zinatoa mapendekezo, lakini hayafanyiwi kazi.

"Sifurahii sana tume ikiundwa, ninaona ni kunyamazishwa, huwa sioni matokeo ya tume hizi. Ngorongoro kuna changamoto kubwa, kama kweli watafanya kazi watakuja na mapendekezo yanayotekelezeka kabisa," alisema.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.***



Ndege ya Shirika la Ndege (ATCL), ikipokelewa kwenye uwanja ndege wa kimataifa wa Oliver Tambo Afrika Kusini, juzi, baada ya kuanza safari zake nchini humo. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Risiti feki za EFD zashtua miradi ya taasisi za serikali

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Morogoro imesema lipo wimbi la risiti za kielektroniki zisizo halisi (feki) zinazotolewa kwenye miradi inayotekelezwa na taasisi za serikali huku baadhi ya wanaofanya mchezo huo wakiwa wazabuni na makandarasi mkoani humo.

Imesema risiti hizo zisizo sahihi mara nyingi pia zimekuwa zinatolewa yanapofanyika malipo ya ununuzi kutoka kwa watoa huduma mbalimbali na kusababisha serikali kushindwa kupata kodi yake.

Meneja Msaidizi wa TRA Mkoa wa Morogoro, Chacha Gotora alisema mwishoni mwa wiki mjini hapa kuwa baada ya kupata malalamiko hayo kutoka taasisi za serikali, wameamua kutoa mafunzo ya kuhakiki risiti sahihi kabla hawajafanya malipo yoyote kwa watoa huduma.

"Kuna baadhi ya kesi ambazo tulikuwa tukizipata kutoka kwa wenzetu wa taasisi za umma kuja kuhakiki risiti na zikaonekana kuna wimbi la kupelekewa risiti zisizo sahihi, hivyo kama TRA tumeamua kutoa elimu kwa viongozi wa taasisi hizo ili wajue risiti sahihi inatakiwa iweje na vitu vya kuitambua," alisema Chacha.

Alisema mafunzo hayo yatasaidia taasisi hizo za serikali zinazotekeleza miradi mbalimbali kuwabaini wazabuni na watoa huduma wengine wanaotoa risiti feki na kuwachukulia hatua wale watakaobainika kuziandaa.

Julieth Hamza, Mhasibu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), alisema changamoto wanayopata ni uelewa wa wazabuni kuhusu Kodi ya Zuwio pale wanapofanya ununuzi na kukatwa kodi hiyo.

"Kukosekana kwa elimu ya Kodi ya Zuwio kumekuwa kunatusababishia matatizo kwa kuwa mzabuni ukimwambia nimekukata hiyo kodi, hataki kukupa risiti ya jumla ya fedha zote badala yake anatoa risiti ya fedha uliyompa," alisema Julieth.

Ofisa Ununuzi katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Abdulkarim Mushi, alisema changamoto iliyosababisha malipo ya wazabuni kuchelewa ni pamoja na utekelezaji kulingana na bajeti iliyotengwa pamoja na kutaka mahitaji ambayo hayajatengewa bajeti husika na kuchelewesha malipo.

***Kwa maoni: +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.***

# ACT: Tunawajua waliomteka Nondo

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha ACT Wazalendo kimewataka wanaomshikilia Mwenyekiti wa Ngome yake ya Vijana, Abdul Nondo, kumwachia haraka kwani kinajua mmiliki na lilikoegeshwa gari lililotumika kumteka.

Nondo anadaiwa kutekwa na watu wasiojulikana jana alfajiri kwenye Stendi ya Mabasi ya Magufuli, iliyoko Mbezi Loius, wilayani Ubungo, Dar es Salaam.

Jeshi la Polisi limesema linachunguza tukio hilo ili kubaini waliomchukua Nondo, wakitumia gari lenye rangi nyeupe aina ya Toyota Landcruizer.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Naibu Katibu wa Haki za Binadamu na Vyombo vya Uwakilishi wa Wananchi wa chama hicho, Mbarala Maharagende, Nondo alitekwa alfajiri ya jana na watu wasiojulikana, akitokea mkoani Kigoma alikokuwa sehemu ya viongozi wa kitaifa walioongoza kampeni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mikoa ya magharibi mwa nchi.

Maharagande alidai Nondo aliwasili Stendi ya Mabasi ya Magufuli kwa usafiri wa basi la Saratoga lenye namba za usajili T 221 DKB.

"Mashuhuda wa tukio wamesema kuwa kulikuwa na purukushani katika utekaji wa Nondo iliyosababisha begi lake dogo la nguo na pingu iliyobebwa na mmoja wa watekaji kudondoka.

"Katibu Mwenezi Mkoa wa Dar es Salaam,Monalisa Ndala na Ofisa wa Harakati na Matukio Taifa, Wiston Mogha, waliofika mapema kituoni huko walitambua haraka kuwa aliyetekwa ni Abdul Nondo kwa sababu walizitambua nguo zake kwenye begi lililodondoka na notebook yake," alisema Maharagande.

"Chama kinaendelea kufuatilia taarifa zaidi kuhusu tukio hili na kitatoa taarifa zaidi kwa umma. Katika hatua ya sasa tunamtaka Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), Cammilius Wambura, kufuatilia haraka tukio hili na kuhakikisha Abdul Nondo anaachiwa huru mara moja," aliongeza.

Hata hivyo, Kiongozi mstaafu wa chama hicho, Zitto Kabwe, alimtaja kwa jina mmiliki wa gari hilo linalodaiwa kutumika katika utekaji huo.

"Tunataka Abdul Nondo aachiwe huru mara moja akiwa mzima wa afya. Tafadhali sana, gari inadaiwa 'parking' (maegesho) na tumejua kila mahala gari hiyo inaegeshwa, mwacheni Nondo haraka iwezekanavyo," alisema.

Msemaji wa Jeshi la Polisi, DCP David Misime, katika taarifa yake kwa umma jana, alisema tayari jeshi hilo linafuatilia tukio hilo.

"Jeshi la Polisi lingependa kuujulisha umma kuwa Desemba Mosi mwaka huu, majira ya saa 11 alfajiri, katika eneo la Stendi ya Magufuli, Mbezi Louis, Dar es Salaam, kuna mtu mmoja mwanamume amekamatwa kwa nguvu na kuchukuliwa na watu waliokuwa wakitumia gari lenye namba za usajili T 249 CMV aina ya Landcruser rangi nyeupe.

"Ilielezwa na mashuhuda kuwa katika purukushani za ukamataji, begi dogo lilidondoshwa na baadhi ya vitu vilivyokuwamo vimetambuliwa ni vya Abdul Omary Nondo.

"Ufutiliaji wa tukio hilo ulianza mara tu ya kupokewa kwa taarifa hiyo polisi, sambamba na kufungua jalada," alisema DCP Misime.

Mnamo mwaka 2018, Nondo, akiwa mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), alitoweka katika mazingira yenye utata, akituma ujumbe kwa baadhi ya jamaa zake, akidai alikuwa ametekwa.

Hata hivyo, Jeshi la Polisi lilimkamata mkoani Iringa, likidai alijiteka ilhali alikuwa kwa mpenzi wake. Alifunguliwa mashtaka ya kujiteka mahakamani, lakini alishinda kesi hiyo. Hata alipokatiwa rufani mwaka 2019, alishinda tena.

Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), Onesmo Olengurumwa, akizungumza na Nipashe jana kuhusu madai ya kutekwa kwa Nondo, alisema:

"Tunalaani vikali matukio ya utekaji yanayoendelea, tunaendelea kuwasiliana na vyombo vya usalama, matukio yote hatupati majibu, tunasikitishwa sana! Tunalaani ila tunahitaji kujipanga kama taifa, tutaendelea kutoa matamko zaidi baada ya kupata taarifa za kina."

Alisema wamekuwa wanamwambia Rais Samia Suluhu Hassan kuwa matukio ya utekaji nchini yanahitaji tume huru na watu huru kuyafuatilia kuliko hali ilivyo. Wanaomba tukio hili limguse ili aunde tume hiyo.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.***



TANGAZO


yas
tigo pesa
sasa ni Mixx
By yas
Ni wakati wetu
www.yas.co.tz
Customer Service: 100

TANGAZO


yas
tigo
sasa ni Yas
Ni wakati wetu
www.yas.co.tz
Customer Service: 100
182757

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga geuzeni ugenini kuwa zaidi ya nyumbani CAF

**WAWAKILISHI** wa Tanzania kwenye mechi za kimataifa, Simba na Yanga mwishoni mwa wiki hii wote watakuwa nchini Algeria kwa ajili ya kuiwakilisha nchi kwenye michezo ya Kombe la Shirikisho na Ligi ya Mabingwa Afrika.

Mabingwa wa Tanzania Bara, Yanga, Jumamosi itakuwa kwenye mji wa Algiers kucheza mechi ya raundi ya pili Kundi A, Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya MC Alger, utakaopigwa,saa 4:00 usiku, Uwanja wa Julliet wa Tano.

Simba itacheza mchezo wake wa raundi ya pili ya Kombe la Shirikisho wa Kundi A, dhidi ya CS Constantine, Jumapili kwenye mji wa Constantine, saa 1:00 usiku kwenye Uwanja wa Mohamed Hamlaoui.

Tunazitakia kila la heri timu hizi za Tanzania zilizobaki kwenye michuano hiyo, lakini tukizikumbusha kuwa hazitakuwa mechi rahisi, hivyo zinatakiwa kwenda kwa tahadhari na kupambana vilivyo zaidi ya zilivyofanya nyumbani.

Tukianza na Yanga, viongozi na wachezaji wanapaswa kufuta kipigo walichokipata kwenye mechi ya kwanza cha mabao 2-0 dhidi ya Al Hilal kwenye mawazo yao na kuufanya Uwanja wa Julliet wa Tano kuwa kama wao wa nyumbani kwa kushambulia mwanzo mwisho, kwani inakwenda kucheza na timu ngumu, ambayo katika mchezo uliopita ililazimisha suluhu dhidi ya TP Mazembe nchini Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

Timu za Afrika Kaskazini, maarufu kama kwa 'Waarabu', kwa miaka mingi zina utamaduni wa kusaka sare ugenini na kuhakikisha zinashinda nyumbani, hivyo, Yanga itabidi iende kwa tahadhari kubwa, icheze kwa mkakati, ili kupata ushindi ama angalau sare na kuepuka kufungwa mechi ya pili mfululizo katika michuano hiyo.

Kingine ni kwamba wachezaji wawe makini, nje na ndani ya uwanja, wawe tayari kukabiliana na vitimbi vya mashabiki wa timu za huko, ambao wanashangilia kupita kawaida na wana asili ya ukorofi na uwezo wa kuwatoa wapinzani wao mchezoni.

Kwa upande wa Simba, sina shaka sana na wachezaji wao kwani pamoja na kwamba wameshapata kashikashi za mechi nyingi za 'Waarabu' ndani na nje ya uwanja kwa miaka kadhaa, lakini hata baadhi ya wachezaji wao wapya, wameonja kidogo hali hiyo walipokutana dhidi ya Al Ahli Tripoli ya Libya ambapo walifanyiwa vurugu iliyowalazimisha wao kuja nchini wakikodisha mabaunsa kwa ajili ya kuhofia Simba kulipa kisasi.

Nadhani pia walipata picha ya kile walichokiona ndani ya uwanja jinsi mashabiki wao wanavyoshangilia.

Tunachowatahadharisha Simba ni kwamba wasithibutu kucheza kama walivyofanya dhidi ya Bravo do Maquis, Jumatano iliyopita kwani na wao wanapaswa kwenda kuugeuza Uwanja wa Mohamed Hamlaoui kuwa kama wao wa nyumbani kwa kuwakimbiza wenyeji wao mwanzo mwisho. Licha ya kushinda bao 1-0, lakini Simba haikuwa kwenye kiwango bora, huku wachezaji wengi wakitaka kupata umaarufu kupitia mechi hiyo. Kila mmoja alitaka kuwa yeye ndiye shujaa akitaka kufunga yeye, hivyo timu kukosa muunganiko. Tuwakumbushe kuwa mashabiki wa soka wa kisasa ambao wanaangalia kwenye televisheni mipira ya nje, hasa Ulaya, wamekuwa na uelewa sana wa soka kiasi kwamba wanatambua mchango wa kila mmoja kwenye kikosi hata kama hajafunga bao.

Lakini pia ikumbukwe Simba ilikuwa na mchezaji, Clatous Chama ambaye kwa sasa yupo Yanga. Huyu hakuwa mfungaji sana, lakini aliheshimiwa na kuwa staa mkubwa kwa sababu ya kutoa pasi za mwisho tu.

Alikuwa akifanya hivyo hata pale ambapo yeye mwenyewe angeweza kufunga. Hivyo, wachezaji wa sasa wa Simba wanachotakiwa ni kuwa na ushirikiano, kila mmoja acheze kwa ajili ya timu na si kupata sifa binafsi. Kwenye michuano mikubwa kama hii, nafasi hupatikana chache na zinapaswa kutumika vizuri.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# RC Tabora aungwe mkono vita upangaji matokeo michezoni

Na Adam Fungamwango

**MKUU** wa Mkoa Tabora, Paul Chacha, amesema atawachukulia hatua kali za kisheria, wachezaji wa timu ya Tabora United watakaobainika kupanga matokeo kwenye mchezo huo wa soka.

Wakati akiipongeza Tabora United kwa mwendelezo mzuri wa michezo mbalimbali, alisema hatovumilia pale atakapogundua kuwa kuna kiongozi wa timu hiyo amefanya mawasiliano na kiongozi wa timu nyingine kwa ajili ya kuuza mechi, kwani si tu kwamba timu yake itaathirika, bali inashusha kiwango cha soka nchini kwa kuwapata washindi ambao hawatokani na uwezo wao.

"Timu inalelewa vizuri, wachezaji hawana shida ya mishahara wala posho, kila kitu wanapata kwa wakati, hatutaki kusikia mechi imeuzwa.

"Tukija kusikia kiongozi fulani amefanya makubaliano na kiongozi wa timu fulani na wameuza mechi, au mchezaji, tutafanya uchunguzi, ikithibitika hatutaviachia vyombo vya soka pekee, na sisi tutachukua hatua za kisheria, tutampeleka mahakamani tukiwa na ushahidi wote na atakwenda jela. Tumeelewana? Hatuwezi kuwaletea mzaha watu wa Tabora hapa, hatutaki mzaha, watu wanataka mpira, wanapenda mpira ni lazima tuwafurahishe, tumeelewana?" Alihoji Mkuu wa Mkoa huyo.

Wakati Chacha akisema hayo, Shirikisho la Mpira wa Miguu chini (TFF), limetoa taarifa ya kuwataka wadau wa michezo kutoa maoni ya kupinga vitendo vya upangaji matokeo kwenye mpira wa miguu.

TFF, imetoa namba za barua pepe, integrity@tff.or.tz, kwa wadau wote wa soka nchini watakapoona au kupata taarifa zozote za upangaji wa matokeo.

**Wakati Chacha akisema hayo, Shirikisho la Mpira wa Miguu chini (TFF), limetoa taarifa ya kuwataka wadau wa michezo kutoa maoni ya kupinga vitendo vya upangaji matokeo kwenye mpira wa miguu.**

Ina maana yoyote kwenye taarifa, ushahidi, awasiliane na TFF kupitia barua pepe hiyo.

Nianze kwa kumpongeza Mkuu wa Mkoa wa Tabora kwani ameonesha ni mwanamichezo wa kweli, akitaka timu yake icheze mpira, ushinde kihalali na kupoteza kihalali.

Ingawa imekuwa ikifichewafichwa kwa kisingizio cha kutokuwa na ushahidi, lakini ni ukweli usiopingika kuwa kuna wakati ligi yetu imekuwa na makandokamndo mengi ya upangaji wa matokeo.

Na mpaka inasemwa na watu wakubwa kama hao, pia TFF kutoa taarifa hiyo, ina maana jambo hili lipo.

Niseme tu kuwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora, anapaswa kuungwa mkono wa wakuu wote wa mikoa na viongozi wote wa soka nchini.

Kama kila mmoja akiamua kufanya kama Chacha, kufuatilia mienendo ya wachezaji na viongozi tena kwa kutumia vyombo vya kisheria, soka letu litakuwa juu ya hapa lilipo.

Timu inatakiwa kushinda kwa uwezo wake, si kusaidiwa kununuliwa mechi, au kiongozi kuamua kuiathiri kisaikolojia timu pinzani na kuitoa mchezoni.

Nadhani kuanzia sasa kila kiongozi wa mkoa, awe makini na timu iliyo kwenye mkoa wake ili kuzuia mchezo huo mbaya. Kwa upande wa TFF, nadhani barua pepe bado haitoshi. Kwa Watanzania si wengi wenye barua pepe. Waliokuwa nazo wengi ni watu wa maofisini tu huku, wadau wengi wa soka ni watu wa kawaida tu mitaani.

Na hao mara nyingi huwa na taarifa nyingi za upangaji wa matokeo na zingine zinazofanana na hizo.

Nawashauri TFF watoe pia namba za simu, ili mashabiki wengi watoe taarifa za upangaji matokeo, au ushauri jinsi gani ya kufanya ili kuepukana na kadhia hiyo.

## MATANGAZO


KILIMANJARO
DRINKING WATER
A PRODUCT OF
The Coca-Cola Company
Mshindi wa
SUPERBRANDS
AFRIKA MASHARIKI
2022-2024
VOTED
Superbrands
EAST AFRICA'S CHOICE
2022-2024
Asanteni wateja wetu
Hii ni yetu sote
kilimanjaro_drinking_water
kilimanjarodrinkingwater
kdw@bbl.co.tz
+255 762628166 | +255 659785276 | +255 272754422

# MATANGAZO

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**INATANGAZWA TENA: MAOMBI YA TAARIFA YA KUONESHA NIA: MPANGO WA UREJESHAJI STAHILI ZA WAGUSWA WA BOMBA LA MAFUTA: UTEKELEZAJI WA MPANGO WA KUENDELEZA UFUGAJI BORA WA NYUKI. NA: REQ 00000620**

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) LTD ("EACOP LTD") inaalika kampuni au mashirika yenye uzoefu na sifa nzuri kuleta maombi yakuonyesha nia yao ya kubuni na kutekeleza Mpango wa ufugaji bora wa Nyuki kwa kaya zilizoathiriwa na mradi wa EACOP.

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la chini ya ardhi linalovuka mipaka kwa ajili ya kusafirisha mafuta ghafi kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda hadi pwani ya mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kuuza kwenye masoko ya kimataifa. Bomba hilo litaanzia Kabaale, Wilaya ya Hoima nchini Uganda hadi rasi ya Chongoleani mkoani Tanga, Tanzania, likipitia katika mikoa nane – Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga, halmashauri za wilaya 27 na vijiji 231.

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA HUDUMA:**

EACOP inatekeleza mipango ya urejeshaji wa maisha kwa Kaya zilizoathiriwa na Mradi (PAHs). Mradi wa EACOP uko mbioni kuanza utekelezaji wa Mpango wa Ufugaji Nyuki ulioboreshwa kwa kaya za waguswa takribani katika wilaya 10 ambapo shughuli za ufugaji nyuki zinafaa. Ubunifu wa mpango huu uko katika hatua za mwisho na huenda ukajumuisha lakini hauishii katika:

- Ushirikishwaji wa kaya ili kuthibitisha uwezo wao wa kuwa sehemu ya mpango.
- Uainishaji wa kaya kulingana na miundo ya mpango.
- Mafunzo juu ya uzalishaji wa mizinga ya nyuki ya kisasa iliyo boreshwa.
- Utafutaji na usambazaji wa vifaa vya ufugaji nyuki na mavazi ya kujikinga yanayofaa kwa nyuki wa Tanzania.
- Mafunzo na kujenga uwezo wa kaya juu ya masuala yote muhimu ya ufugaji nyuki, ikijumuisha mafunzo ya awali na ya juu ya ufugaji nyuki, aina za mizinga zinazopendekezwa, muundo na ukarabati wa mizinga, vifaa vinavyohitajika, uwekaji bora wa mizinga, na mbinu bora za kukusanya, kuchakata na kuvuna asali.
- Msaada katika kuandaa kalenda za msimu wa uzalishaji wa asali.
- Kuanzisha uhusiano na sekta binafsi kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa masoko na uwezekano wa uwekezaji katika uzalishaji wa asali katika wilaya zilizoathiriwa na Mradi.
- Kusaidia upatikanaji wa fursa za kuongeza thamani ya mazao ya Nyuki.
- Huduma za ughani kwa kaya kwa kipindi cha mwaka mmoja.

**VIGEZO MUHIMU:**

**Mashirika yenye nia yanaalikwa kuandika ombi lao na:**

- Maelezo ya miradi sawa au shughuli zilizofanywa, ambazo zinatoa ushahidi wa timu yenye sifa na inayopatikana, uzoefu kwenye mikoa inayopitiwa na mradi wa Bomba, na rekodi ya kufuatilia ya uzoefu ulioorodheshwa hapo juu.
- Uthibitisho wa sifa na utayari wa timu yenye rekodi bayana ya ushiriki katika programu za ufugaji bora wa nyuki.
- Uthibitisho wa usajili na Asasi husika za Usajili Tanzania (BRELA, NGO Registration, OSHA).
- Uthibitisho wa usajili na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha kuidhinisha Kodi kwa mwaka wa hivi karibuni unaopatikana.
- Muonyesha nia awe amekwisha jisajili au amekwisha tuma maombi yaliyoidhinishwa kusajiliwa katika kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani.
- Uthibitisho wa taarifa za Ukaguzi wa hesabu wa kampuni za hivi karibuni.
- Ushahidi wa mfumo wa Usimamizi wa Ubora, Afya, Usalama, na Mazingira (QHSE), shirika, na mchakato kwa kufuata viwango vya Serikali na Viwanda vinavyotumika kwa kazi sawa.
- Uthibitisho wa sera za kupambana na rushwa, kupambana na kutoa hongo, kuzingatia sheria na haki za binadamu.

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia **saa 11:00** jioni Majira ya Afrika Mashariki, **tarehe 20 Disemba 2024**. Kichwa cha Barua Pepe kiwe: **Maombi ya kutekeleza Mpango wa ufugaji bora wa Nyuki. Maombi yote yakuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20.** Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kiingereza.

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yaliyoonesha nia kulingana na Tangazo hili la Nia ya kutoa Huduma, na kisha kufanya tathmini kulingana na vigezo vya ndani vya EACOP ili kubaini makumpuni yenye sifa yatakayojumuishwa kwenye orodha ya awali ya makampuni yenye vigezo. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA). Kampuni ya EACOP LTD ina haki ya kuteua au kukataa kampuni na kubaki na maamuzi yake bila ya kutoa sababu kwa kamapuni husika.

182745

TEMBO NICKEL

# VACANCY

## FINANCE LEAD-DAR ES SALAAM

**Position Summary:**
Tembo Nickel is seeking to recruit the Finance Lead to join the Kabanga Nickel Project Team. The successful candidate will be responsible for driving the project from a financial point of view, including budgeting, cost allocation, reporting, and governance.

The successful candidate will report to the **Chief Financial Officer (CFO)**

**Duty Station: Corporate Office-Dar es Salaam**

**Key focusing areas will include:**

- Corporate financial reporting and creation of statutory accounts.
- Day-to-day ownership of accounting functions, including month-end close.
- Cost and management reporting to site and Group based in London.
- Internal control and SOX compliance management.
- Management of local and Group audit timelines.

**Duties and Accountabilities**

- Responsible for the timely and accurate preparation of financial statements and other financial reports, ensuring the accuracy of financial reporting for local companies and reporting to the Group.
- Ensure financial governance, internal controls, and SOX compliance by Group standards are always maintained.
- Ensure that all internal and external reporting deadlines are met at all times.
- Responsible for producing timely monthly cost centre management accounts and qualitative commentary against the approved budget.
- Assist the CFO in preparing budgets, forecasts, and presentations to local and Group management.
- Ensure all day-to-day, month-end financial accounting tasks are timely (e.g. reconciliations, legal filings and relevant documentation).
- Assist the CFO in driving standardization of processes between Group and project sites.
- Identification and reporting of accounting issues and supporting the development of documentation of standard operating procedures (SOPs) in line with the group standards.
- Facilitate the coordination of the CFO and integrated planning meetings with Heads of Department.
- Review operating capital expenditure and forecasts to ensure alignment with business strategy and to optimize return on investment.
- Assist the CFO in initiating, developing, implementing, streamlining, and maintaining the company's necessary financial strategies, policies, and procedures to manage finances effectively.
- Ensure adherence to legislative and corporate governance compliance requirements.
- Communicate findings of audits, best practices, and improvement recommendations to senior management.
- Lead, mentor and manage the finance team through hands-on management and applying industry best practices.

**Qualifications and Competencies**

The applicant should have:

- A degree from a recognised higher learning institution in Accounting and Finance, Economics, or another relevant field.
- Professional Accounting qualification, preferably CPA and ACCA
- At least eight (8) years of experience with a global audit firm.
- Worked in a listed company.
- SOX experience ideal.
- Proficiency in audit processes, financial reporting and IFRS reporting standards.
- Strong Excel skills and familiarity with financial software.
- Experience with the mining industry.

**Behavioural Skills**
The applicant should have the following skills:

- Proven project management skills in a multicultural environment.
- Hard working and ability to work in small, dynamic and young organizations.
- Hands-on ability to engage directly with tasks, tools and processes, with minimal supervision.
- Excellent problem-solving and analytical skills that effect positive change.

Tembo Nickel offers a competitive remuneration package, and ONLY shortlisted candidates will be contacted.

**How to Apply**
Applicants are invited to send their resumes indicating the role title in the subject via email **jobs@tembonickel.com.** The application closing date is 13th December 2024

Note: We are committed to provide equal employment opportunities based on merits, and we do not charge candidates any fees during the whole recruitment process
**Women are strongly encouraged to apply.**

**For and on behalf of Tembo Nickel, the Kabanga Nickel Project**

182748





**HABARI KASKAZINI**

# Mchakato kupandisha viwango vya ufaulu waanza

**Na Getrude Mpezya,** ARUSHA

SERIKALI imeanza kuwanoa wadhibiti ubora wa elimu ambao watafanya kazi ya kupandisha viwango vya ufaulu na kuzalisha wanafunzi wa masomo ya amali.

Mkurugenzi Uthibiti Ubora wa Shule wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Ephrahim Simbeye, akizungumza mwishoni mwa wiki Jijini Arusha, alisema walengwa wa mafunzo hayo wanatarajia kuchochea mabadiliko katika sekta ya elimu nchini.

"Tumewaleta kujinoa kuhusu elimu ya amali ili kuwawezesha kuboresha kiwango cha elimu ya vitendo na kuzalisha wanafunzi watakaoweza kujitegemea kimaisha baada ya kumaliza masomo.

"Niwasihi wathibiti ubora kuwasikiliza kwa umakini watoa mada ili elimu hiyo iwasaidie na wengine waliobaki ofisini kwa lengo la kuboresha kiwango cha elimu na kuingia katika mashindano ya kikanda na kidunia.

...Ndugu zangu nyinyi ndiyo watu wa viwango wa elimu yetu na jiicho la Wizara. Mkishirikiana na kukaa pamoja naamini mabadiliko yatakuwa makubwa; tunategemea mafunzo haya yawe endelevu na yenye kuleta tija, msiwe wachoyo wa kuwaelimisha wengine ili kufikia malengo ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kama inavyotakiwa." alisema

**"Nawakumbusha kutembelea vivutio vya utalii vilivyopo hapa Mkoa wa Arusha ili kuliingizia taifa mapato, hii inawezekana kukifanyika utaratibu mzuri ili mkafurahie**

Hatahivyo, aliwataka kuthibiti ubora wa ndani ya shule, kushirikisha jamii katika masuala ya maendeleo ya elimu, kusimamia unasihi na ushauri nasaha kama ilivyo katika suala la maadili.

"Nawakumbusha kutembelea vivutio vya utalii vilivyopo hapa Mkoa wa Arusha ili kuliingizia taifa mapato, hii inawezekana kukifanyika utaratibu mzuri ili mkafurahie mandhari na utajiri uliopo katika vivutio hivyo" alisema Simbeye.

Kwa upande wake Mkurugenzi Msaidizi Elimu ya Ualimu, Huruma Mageni alisema mafunzo hayo ni muhimu kutokana na umuhimu wa elimu ya amali inayolenga kuleta chachu na matokeo makubwa katika teknonojia na kujitegemea.

"Pongezi zetu ziwaendee wawezeshaji na maofisa kamisheni kutoka Wizara ya Elimu, NACTEVATE na VETA watakao fundisha mpangilio na mtaala wa amali na fani za amali, utaratibu wa kusajiri shule za amali, muundo wa kuandika tathmini ya amali na mengine mengi" amefafanua Mageni.

Mthibiti Ubora Elimu wa Halmashauri ya Wilaya Newala mkoani Mtwara, Rashid alisema wawezeshaji wameanza kutoa mwanga na maelekezo kuhakikisha elimu ya amali inaboreshwa.

"Kwa upande wangu changamoto ninazoziona ni upungufu wa walimu katika shule za amali, vifaa vya kufundishia na miundombinu michache kwa maana ya maktaba na maabara" alisema Rashid.

Mthibiti Ubora kutoka Halmashauri ya Handeni Mkoani Tanga, Telesia Kapinga alisema mafunzo hayo yatawapatia elimu ya kujitegemea na kuanzisha viwanda vidogovidogo.

Mafunzo hayo yatafungwa Desemba 02 na yamebeba kaulimbiu isemayo "Utoaji wa elimu bora ya amali hutegemea tathmini makini ya ufundishaji na ujifunzaji".

# Utafiti, uchimbaji visima vya maji kufanyika Manyara

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

SERIKALI imepanga kuanza kutekeleza miradi mipya 32 ya ukarabati, ukaguzi, utafiti na uchimbaji wa visima virefu vya maji mkoani Manyara.

Leng oni kukabiliana na makali ya mgawo wa maji unaotokana na vyanzo vichache vya maji.

Miradi hiyo itatekeleza katika bajeti ya mwaka wa fedha 2024/25, ikiwa na thamani ya Sh. bilioni 77.3

Kaimu Meneja wa Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA), mkoani humo, James Kionaumela, alisema mpango huo unatokana na wastani wa uzalishaji wa maji kwenye skimu 209 za mkoa huo, kuzalishwa lita 42,000.7 kwa siku.

"Kwa sasa kuna miradi 22 yenye thamani ya shilingi bilioni 90.9 inaendelea na utekelezaji na miradi 32 mipya ya ukarabati, ukaguzi, utafiti na uchimbaji wa visima kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2024/25 yenye thamani ya shilingi bilioni 77.3, ndiyo inategemea kuanza kujengwa mwaka huu," alisema.

Meneja huyo, alisema kati ya vijiji 440 vya mkoa huo, RUWASA inahudumia vijiji 396, ambapo kati ya hivyo, vijiji 277 vina maji ya mtandao na vijiji 52 vinatumia pampu za mkono na umeme wa jua (sola).

Vilevile, alisema upatikanaji wa maji vijijini ni asilimia 75 na wakazi wanaohudumiwa ni milioni 1.5, ambapo wenye maji ni wananchi milioni 1.06.

Katika hatua nyingine, Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, alisema kwa mwaka wa fedha 2023/24 mkoa umepokea Sh. bilioni 190 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ya sekta mbalimbali zikiwemo maji, afya, elimu, utawala, uwekezaji, biashara, kilimo na nishati.

Sendiga, alisema kwa sekta ya elimu imejengwa shule ya sayansi ya wasichana na shule ya wavulana inajengwa hadi Desemba itakamilika.

Pia, alisema katika shule za msingi mkoani humo madarasa 249 matundu ya vyoo 389, maabara 14 yamejengwa.

Kuhusu afya, Sendiga alisema zimejengwa zahanati 19, vituo vya afya 11, ununuzi wa vifaa tiba katika hospitali mbili za wilaya.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA WILAYA
KINONDONI
SHAURI LA MAOMBI MADOGO NAMBA 26715 MWAKA 2024
KUMBUKUMBU NAMBA. 202410241000026715

CONTRACTORS REGISTRATION BOARD CRB..........................................MDAI

DHIDI YA

MAJOR CONSULTANTS LIMITED.........................................................1 MDAIWA
NINA JIHADGAR KINGO.....................................................................2 MDAIWA
JOHN MOSES MBWANA.....................................................................3 MDAIWA

Kwa:

JOHN MOSES MBWANA:

KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa Mdai ameleta maombi yake madogo ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala zake za maombi madogo ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo unahitajika kuhudhuria Mahakama hii binafsi au Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa siku ya **JUMANNE** Tarehe **03 Mwezi 12 Mwaka 2024 Saa 5:00 Asubuhi Mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi J.J.RUGEMALILA.**

Kwa mujibu wa Maombi hayo, na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kutaja kwa kesi hiyo.

ANGALIZO:

Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kama umepokea wito wa kuitwa shaurini.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe **29 Mwezi 11 Mwaka 2024.**

RESIDENT MAGISTRATE
KINONDONI DISTRICT COURT
DAR ES SALAAM

Hakimu Mkazi
Mahakama Ya Wilaya Kinondoni



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA WILAYA
KINONDONI
SHAURI LA MAOMBI MADOGO NAMBA 26715 MWAKA 2024
KUMBUKUMBU NAMBA. 202410241000026715

CONTRACTORS REGISTRATION BOARD CRB..........................................MDAI

DHIDI YA

MAJOR CONSULTANTS LIMITED.........................................................1 MDAIWA
NINA JIHADGAR KINGO.....................................................................2 MDAIWA
JOHN MOSES MBWANA.....................................................................3 MDAIWA

Kwa:

MAJOR CONSULTANTS LIMITED:

KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa Mdai ameleta maombi yake madogo ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala zake za maombi madogo ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo unahitajika kuhudhuria Mahakama hii binafsi au Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa siku ya **JUMANNE** Tarehe **03 Mwezi 12 Mwaka 2024 Saa 5:00 Asubuhi Mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi J.J.RUGEMALILA.**

Kwa mujibu wa Maombi hayo, na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kutaja kwa kesi hiyo.

ANGALIZO:

Kama hukuhudhuria siku iliyo'ajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kama umepokea wito wa kuitwa shaurini.



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA WILAYA
KINONDONI
SHAURI LA MAOMBI MADOGO NAMBA 26715 MWAKA 2024
KUMBUKUMBU NAMBA. 202410241000026715

CONTRACTORS REGISTRATION BOARD CRB..........................................MDAI

DHIDI YA

MAJOR CONSULTANTS LIMITED.........................................................1 MDAIWA
NINA JIHADGAR KINGO.....................................................................2 MDAIWA
JOHN MOSES MBWANA.....................................................................3 MDAIWA

Kwa:

NINA JIHADGAR KINGO :

KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa Mdai ameleta maombi yake madogo ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala zake za maombi madogo ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo unahitajika kuhudhuria Mahakama hii binafsi au Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa siku ya **JUMANNE** Tarehe **03 Mwezi 12 Mwaka 2024 Saa 5:00 Asubuhi Mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi J.J.RUGEMALILA.**

Kwa mujibu wa Maombi hayo, na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kutaja kwa kesi hiyo.

ANGALIZO:

Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kama umepokea wito wa kuitwa shaurini.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe **29 Mwezi 11 Mwaka 2024.**

RESIDENT MAGISTRATE
KINONDONI DISTRICT COURT
DAR ES SALAAM

Hakimu Mkazi
Mahakama Ya Wilaya Kinondoni





# CRDB yashinda tuzo ya chaguo namba moja, bunifu kwa wateja

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB imeanza mwezi Desemba kwa kushinda tuzo mbili kutambua juhudi zake za kukidhi mahitaji na matarajio ya wateja wake kote nchini.

Tuzo hizo zilizotolewa na Consumer Choice Awards Africa (CCA) 2024, zimezingatia maoni ya wateja na wadau tofauti walioshirikishwa na kupiga kura kumchagua mtoa huduma bora.

Benki ya CRDB imenyakua tuzo ya benki chaguo namba moja ukanda wa mashariki mwa Afrika kutokana na urahisi wa kufikika pamoja na tuzo ya benki yenye promosheni bunifu inayowanufaisha wateja wake. Akikabidhi tuzo hizo mbili, Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji, Stanslaus Nyongo alisema mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam kuwa ushindi huo unatokana na juhudi makini za kuhudumia soko.

"Ninaawapongeza sana. Juhudi zenu zinaonekana kwa namna mnavyowahudumia wateja na kushirikiana na wadau tofauti kuongeza ubunifu wenye tija. Hongereni sana Benki ya CRDB," alisema Nyongo.

Akipokea tuzo hizo, Ofisa Mkuu wa Biashara wa Benki ya CRDB, Boma Raballa alisema ubunifu unaomzingatia mteja ndio msingi wa huduma za Benki ya CRDB kila siku, hivyo ni furaha kuona jamii inalitambua hilo.

"Sisi ni benki inayomsikiliza mteja. Wateja wetu waliosambaa nchi nzima wana mahitaji tofauti ambayo tunajitahidi kadri ya uwezo wetu kuyakabili. Kwa walio mbali na tawi, tunawasogezea na wale wanaohitaji huduma mahali popote walipo na wakati wowote tunawapa wanachokitaka. Tunaamini mteja akifurahi, biashara yetu itakuwa endelevu," alisema Raballa.

**"Kila mwaka tunakuwa na Benki ya CRDB. Kura za wateja ndizo zinazoipa ushindi kutokana na jinsi wanavyoridhishwa na huduma inazozitoa," alisema Diana.**

Kuhusu tuzo ya benki bora inayopendwa, inayopatikana popote na rahisi kufikika ukanda wa mashariki mwa Afrika (the most preferred, convenient, and accessible bank in eastern Africa), Raballa alisema Benki ya CRDB inaongoza kwa mtandao mpana wa matawi ambayo ni zaidi ya 260 yaliyopo katika halmashauri zote nchini pamoja na mawakala zaidi ya 25,000 wanaosaidia kutoa huduma.

Na kuhusu tuzo ya benki yenye promosheni bunifu inayowanufaisha wateja wake (the most creative and innovative consumer benefiting campaign of the year) ambayo imeitambua promosheni ya Benki ni SimBanking; miamala inalipa swahiba, Raballa alisema ni ukweli ulio wazi kwamba programu ya SimBanking imeleta mapinduzi makubwa kwenye huduma za fedha nchini.

Mwanzilishi na Mkurugenzi Mtendaji wa Consumer Choice Awards Africa, Diana Laizer alisema Benki ya CRDB ni mdau mkubwa wa tuzo hizo na imekuwa inashiriki mara nyingi. "Kila mwaka tunakuwa na Benki ya CRDB. Kura za wateja ndizo zinazoipa ushindi kutokana na jinsi wanavyoridhishwa na huduma inazozitoa," alisema Diana.

Mkuu wa Kitengo cha Huduma kwa Wateja, Yolanda Uriyo alisema wana kituo cha huduma kwa wateja kinachofanya kazi muda wote, wakimsikiliza mteja atakayepiga simu, kutuma baruapepe au barua hata yule atakayewasiliana nao katika akaunti zao za mitandao ya kijamii.



Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo ya Isagehe, Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Latifa Chisanga akiwaapisha wenyeviti wa vijiji, vitongoji na wajumbe wake, kiapo cha uaminifu, kutunza siri, utii na uadilifu, katika kata ya Mwakata, juzi. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Polisi wapiga kambi Tarime kudhibiti ukatili

**Na Ambrose Wantaigwa,** TARIME

JESHI la Polisi limeamua kuhamishia maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili katika mkoa wa kipolisi Tarime/Rorya mkoani Mara, kutokana na kukithiri kwa vitendo vya ukatili ikiwemo ukeketaji katika eneo hilo.

Pia, Jeshi hilo kwa kushirikiana na wadau wa kupinga ukatili wa kijinsia wameeleza kufanikiwa kuwaokoa wasichana 184 waliokuwa wameandaliwa kufanyiwa ukeketaji mwishoni mwa mwaka 2024 wilayani Tarime.

Akizungumza kuhusu kambi hiyo Kamanda wa polisi Tarime/Rorya ACP Mark Njera alisema itahusisha viongozi wa dini, serikali za mitaa, wazazi na wazee wa mila kutoka koo zote eneo hilo.

Kamanda Njera alisema wasichana waliowaokoa wengi ni wanafunzi wa shule za msingi na sekondari na walio chini ya umri wa miaka 18, kwa sasa wamehifadhiwa sehemu salama.

Alisema kwa sasa utaratibu unaandaliwa wa kisheria ili kuwafikisha mahakamani waliohusika.

Alisema lengo la kuweka kambi hiyo katika kanda hiyo maalum ni kuzuia ukeketaji wakati na baada ya maadhimisho hayo, ili kuhakikisha wasichana wote katika eneo hilo wanakuwa salama na kulindwa.

Taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Msemaji wa Jeshi hilo David Misime ilieleza kwamba maadhimisho hayo yalianza Novemba 25, 2024 na yanawaweka pamoja maofisa wakaguzi na askari waliopo katika madawati ya jinsia na watoto kutoka Bara na Zanzibar.

Alisema shughuli zitakazofanyika wakati wa kambi hiyo ni kutoa elimu juu ya madhara ya ukeketaji na ukatili mwingine kwa watoto na wanawake ikiwemo ubakaji, ulawiti na madhara ya ndoa za utotoni.

Akifungua maadhimisho hayo, Mkuu wa Wilaya hiyo, Edward Gowele alisema serikali itachukua hatua kali kwa wazazi wote na mangariba watakaotekeleza vitendo hivyo.

Alibainisha kwamba serikali inachunguza mbinu mpya zinazotumika kukwepa vyombo vya dola wakati wa ukeketaji ikiwa ni pamoja na kuwavisha wasichana nguo za kiume na kuwamwagia damu ya ng'ombe.

# Silaa: Matukio ya ulaghai mtandaoni yamepungua

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Jerry Silaa, amesema matukio ya ulaghai kupitia mitandao ya simu za mkononi yamepungua kutokana na hatua kali za kiusimamizi na juhudi za kuelimisha watumiaji kujilinda.

Alitoa kauli hiyo jana baada ya kukutana na watoa huduma za mawasiliano ya simu za mkononi na wengine wa masuala ya usalama mtandaoni, kwa ajili ya kushauriana hatua endelevu za kumaliza tatizo la uhalifu mtandaoni.

Alisema taarifa ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inaonesha kuwa matukio ya ulaghai mitandaoni yaliyoripotiwa yamepungua kwa asilimia 28 kati ya Juni na Septemba mwaka huu.

Ripoti ya takwimu za mawasiliano inaonesha matukio 16,002 ya ulaghai yameripotiwa Tanzania nzima kati ya Juni na Septemba 2024 ukilinganisha na 22,257 kati ya Aprili na Juni.

Aidha, alisema kutokana na hali hiyo wizara na taasisi zake za mawasiliano kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi wataongeza msukumo kushughulikia usalama mtandaoni.

"Ulaghai unaathiri juhudi za serikali kueneza huduma za jamii na za utawala kupitia mitandao. Vilevile unahujumu mikakati ya kuendeleza ushirikishaji wa wananchi kwenye mifumo ya kifedha na kujenga uchumi wa kidijiti," alisema.

"Uhalifu unaofanyika ni pamoja na kuwalaghai watu kwa kuwapigia simu na kuwatumia ujumbe mfupi, yaani meseji za ulaghai na kuwataka watoe taarifa zinazohusu akaunti zao za pesa kwa simu au za kibenki, miamala, nywila na namba za siri. Hii inawawezesha wahalifu kuiba kwenye akaunti za pesa kwa simu, benki au za wakala wa huduma za pesa mtandao," alifafanua.

Kwa mujibu wa Silaa, asilimia 77 ya matukio kati ya Juni na Septemba yaliripotiwa kwenye mikoa ya Rukwa, Morogoro na Mbeya huku mikoa yenye ripoti chache za ulaghai mtandaoni na idadi kwenye mabano ni Kusini Unguja (6), Kusini Pemba (10), Kaskazini Unguja (12) na Simiyu (16).

Aidha, aliitaka TCRA kuhakikisha wanatoa huduma wanadhibiti taratibu za usajili wa laini za simu kwenye maeneo yote yaliyoonesha viashiria vya juu vya uhalifu.

TCRA inatekeleza mipango ya elimu kwa umma ambapo watumiaji wanaruhusiwa kupiga simu kwa msimbo 15040 wanapokumbana na kadhia ya ulaghai.

Nipashe
# Spotika




WACHEZAJI WAWILI MAPATINA BORA ZAIDI WA SOKA DIMBANI UK. 12-13



MBAPPE

# MADRID: UBORA, KIWANGO NA MATARAJIO MSIMU HUU

VINICIUS

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid imekuwa klabu bora barani Ulaya katika kipindi cha miaka 10 iliyopita, ikishinda mataji mengi ya Ligi ya Mabingwa - ushindi wao wa hivi karibuni zaidi ukiwa ni timu yenye sura mpya iliyojaa vipaji vya hali ya juu - na kujiimarisha kama timu inayoongoza nchini Hispania.

Hata hivyo, baada ya msimu uliopita kushinda mataji mawili, mambo hayajamwendea sawa kocha Carlo Ancelotti.

Kuwasili kwa Kylian Mbappe kumezua utata wa kimbinu, huku tatizo la majeruhi likifichua mapungufu kwenye kikosi chake. Hapa tunaangalia mwanzo wa Madrid kwenye msimu ulivyoenda na kile tunachoweza kutarajia kutoka kwa 'Los Blancos' hao wakati uliobakia wa msimu huu.

### Kiwango cha ubora

Msimu wa Real Madrid ulianza kama unavyoweza kuwa kwa klabu yoyote duniani, ikitwaa UEFA Super Cup dhidi ya Atalanta huku Kylian Mbappe akifunga kwenye mechi yake ya kwanza.

Los Blancos walikwenda bila kufungwa katika michuano yote hadi mapema Oktoba, wakiendelea na mbio za kuwania taji la LaLiga huku Barcelona wakisonga mbele kwa kuwafunga Stuttgart katika mechi yao ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Hata hivyo, kichapo kutoka kwa Lille kilionesha uchezaji wao mdogo kabla ya ushindi wa mechi tatu mfululizo na kujikuta wakichezea kichapo 'hevi' kwenye El Clasico wakati Barca wakiibuka na ushindi wa mabao 4-0 kwenye Uwanja wa Bernabeu.

Kipigo kingine kutoka kwa Milan kiliifanya Madrid sasa kuhisi kuwa na mfumo mbaya wa uchezaji kwa kuwachezesha pamoja Mbappe na Vinicius Junior.

Ingawa walifanikiwa kurejea kwa ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Osasuna kabla ya mapumziko ya kimataifa ya Novemba, majeraha ya Dani Carvajal, Eder Militao, David Alaba na Thibaut Courtois wakiwa ni miongoni mwa wengine, yameonekana kuwa mabaya sana kwao.

### Wachezaji bora

Madrid huwa na wagombea wengi linapokuja suala la mchezaji bora wa msimu, lakini chaguo ni chache zaidi msimu wa 2024/25 kuliko ilivyokuwa kawaida.

Wakati safu ya ushambuliaji bado haijaingia kwenye gia, hakuna shaka kuwa Vinicius Junior ana ubora wa kudumu na umuhimu kwa timu.

Nyota huyo wa Brazil amefunga hat-trick mbili - moja ambayo ilisaidia Madrid kupindua matokeo ya mabao 2-0 dhidi ya Borussia Dortmund - na amekuwa mleta tofauti wakati timu yake ikihitaji ushindi.

Wakati inaonekana kila beki wa karibu naye amepigwa na jeraha, Antonio Rudiger bado amesimama imara.

Mjerumani huyo anaweza kufanya vizuri wakati wa kukosekana kwa matokeo na anabakia kuwa na uhakika kama beki wa kati na hata ana mabao mawili kwenye Ligi ya Mabingwa.

### Kiwango duni

Bado kuna muda mwingi uliobakia msimu huu na kwamba wachezaji hawa hawana haja ya kuhofia kuwa kampeni hiyo itafutiliwa mbali, lakini hakuna shaka kuwa baadhi ya nyota hawajaonesha kiwango bora wanachoweza kufanya, iwe ni kutokana na matatizo ya mfumo au vinginevyo.

Kwa kuzingatia hali yake ya kuwa mchezaji bora zaidi duniani kabla ya uhamisho wake wa bure kutoka Paris Saint-Germain, miezi michache ya kwanza ya Kylian Mbappe akiwa na jezi ya Madrid imekuwa ya kusikitisha.

Akiwa amefunga mabao nane katika mechi 16, nahodha huyo wa Ufaransa ameingia kwenye njia ya Vinicius kwani nyota wote wawili wanapenda kucheza kutoka upande wa kushoto na haonekani kufurahia kabisa kucheza nafasi ya mshambuliaji wa kati.

Jude Bellingham alikuwa akipachika mabao wakati huu mwaka jana, lakini masuala ya Mbappe na Vinicius yamesababisha tishio kwake msimu huu, huku viungo wenzake Aurelien Tchouameni na Federico Valverde wakiwa chini ya viwango vyao vilivyotarajiwa.

### Matarajio ya msimu

Hakuwezi kuwa na uamuzi wa kutwaa mataji inapokuja kwa Real Madrid. Miamba hao wa Hispania ni washindi mfululizo na wamefanya mwanzo mbaya zaidi katika msimu uliopita na bado walipona na kushinda kila aina ya medali.

Hivyo ilisema, haipaswi kupuuza shida zao za hivi sasa. Iwapo Ancelotti hawezi kutafuta njia kwa Vinicius na Mbappe kuishi pamoja na kustawi pamoja, huenda wasimalize kampeni wakiwa kileleni nchini Hispania na Ulaya.

Majeraha katika safu ya ulinzi yanaweza kuharibu kampeni ya Madrid kirahisi, lakini wameonesha ustahimilivu siku za nyuma na unaweza kuonekana mpumbavu ukiwaondoa kwenye mbio zozote za ubingwa msimu huu.

## ISIKUPITE



Si kwamba tu ni hat-trick ya kwanza ya penalti katika zama mpya za Ligi Kuu England (Premier League era), ambayo iliisaidia Bournemouth kushinda mabao 4-2 dhidi ya Wolves katika Uwanja wa Molineux juzi, Jumamosi, bali ilikuwa daraja la juu kwa Justin Kluivert katika jinsi ya kupiga mkwaju wa penalti, hivyo kuifikia rekodi iliyodumu kwa miaka 65 ya Ken Barnes ambaye aliifungia Manchester City kwa penalti katika ushindi wa 6-2 dhidi ya Everton kwenye Uwanja wa Maine Road Desemba 7, 1957.

Extra Time

# WACHEZAJI WAWILI MAPATINA BORA ZAIDI WA SOKA



HARRY KANE NA SON HEUNG-MIN

**LONDON,** England

MAMBO bora mara nyingi huja na vitu viwili, kwa mfano chumvi na pilipili au chai na sukari na hata chips na mayai au chips kuku.

**Kwa kawaida, kumekuwa na vitendo vya kuvutia katika soka kwa miaka mingi, kuanzia ushirikiano wa washambuliaji wa kuvutia hadi 'pea' mbili za ulinzi.**

Ndani ya mchezo wa timu, baadhi hufanya kazi vema wakiwa na ushirikiano wa kuvutia.

Kuunda uhusiano wa wawili kwenye uwanja wa soka si jambo rahisi, na watu wawili waliofanikiwa zaidi wanashirikiana kwa kupata kile kilicho bora kwa timu kwenye kila hatua.

Sasa, makala haya yanakuchambulia baadhi ya wachezaji wawili mapatina dimbani katika historia ya soka.

### Johan Cruyff na Johan Neeskens

Johan Cruyff, mmoja wa waanzilishi wakuu wa 'total football' katika miaka ya 1970, alijikuta kipaji chake kikiwezeshwa na mmoja wa mchezaji mwenzake, Johan Neeskens. Wawili hao walicheza pamoja kwa upatina mzuri zaidi katika muongo mzima, wakichanua katika Klabu za Ajax, Barcelona na Timu ya Taifa ya Uholanzi.

Neeskens alichukua nafasi ya kiungo wa kati ili kuunga mkono ubunifu wa kuvutia wa Cruyff na wawili hao walianzisha uhusiano mzuri walipokuwa wakicheza kwa klabu na nchi. Neeskens alitoa uthabiti na dhamira katika eneo la kiungo na kuwa injini iliyomwezesha Cruyff kufanya anavyotaka pale mbele na kuzinyanyasa vibaya safu za ulinzi za wapinzani.

### Paolo Maldini na Marco Baresi

Ni wachezaji waliokuwa wanashauriana zaidi uwanjani wakiwa AC Milan.

Walikuwa ni mabeki walioelewana zaidi kwa kulinda lango lao kwa umahiri mkubwa zaidi. Wawili hao ilikuwa ni ngumu kuwapenya wakiwa pamoja kwenye klabu na timu ya taifa, kwani walifungwa mara 23 tu katika mechi 196 walizocheza pamoja.

### Alan Shearer na Chris Sutton

Ni muda mrefu tangu Blackburn Rovers ilipokuwa inatawala Ligi Kuu England, huku mafanikio hayo yakichagizwa kwa ushirikiano mzuri zaidi wa Alan Shearer na Chris Sutton.

Wawili hao waliopewa jina la 'SAS', walitengeneza mabao 49 kati yao wakati wa kampeni ya Ligi Kuu msimu wa 1994/95, wakijivunia sifa kali za nguvu za mwili na uwezo wa kumalizia.

### Dwight Yorke na Andy Cole

Dwight Yorke na Andy Cole walicheza pamoja kwa upatika katika timu tatu tofauti.

Mara ya kwanza walicheza kwa upatina mzuri zaidi wa mafanikio makubwa wakiwa pamoja pale Manchester United, ambapo waliwawezesha 'Mashetani Wekundu' hao kutwaa mataji matatu msimu wa 1998/99. Wakifunga mabao 53 kwa pamoja kati yao.

Baada ya Yorke na Cole kustawi pamoja wakiwa Old Trafford, waliungana tena kule Blackburn, ingawa hawakupata mafanikio makubwa zaidi pale Ewood Park.

Hata hivyo, wawili hao bado waliweza kuwa pamoja katika siku zao za mwisho za uchezaji kule Sunderland ambako walimalizia kipindi chao cha uchezaji.

### Robert Pires na Thierry Henry

Robert Pires na Thierry Henry walikuwa mapatina wazuri sana uwanjani na pia marafiki wazuri nje ya uwanja. Wakati walipojiunga na Arsenal walibeba mataji pamoja.

Henry mara nyingi aliongoza vichwa vya habari kwa uchezaji wake wa kutanguliza mpira na kufuata kwa mbio kali, lakini Mfaransa mwenzake alichagua kucheza kwa taratibu akimsukumizia tu pasi. Walifunga kwa pamoja mabao 29 kwenye Ligi Kuu England.

### Alessandro Del Piero na David Trezeguet

Alessandro Del Piero alikuwa tayari amejipatia jina katika Klabu ya Juventus kabla ya kuwasili kwa David Trezeguet mwaka 2000. Hata hivyo, kuingia kwa Mfaransa huyo kuliboresha uchezaji wa Del Piero.

Unyenyekevu wa Del Piero ulikamilisha uwezo wa Trezeguet kikamilifu na wawili hao walitumia muongo mmoja pamoja wakicheza kwa maelewano mazuri sana pale Turin. Kwa pamoja walishinda mengi, yakiwamo mataji mengi ya Serie A - na hata Serie B baada ya kushushwa daraja kutokana na kashfa ya upangaji matokeo.

### Frank Lampard na Didier Drogba

Wawili hawa ni wababe wa muda wote wa Chelsea walishirikiana uwanjani kwa takriban muongo mmoja na walikuwa na nguvu kubwa katika tatu ya mwisho pale London Magharibi. Frank Lampard alikuwa mlishaji mzuri wa mipira kwa Didier Drogba.

Wawili hao walikuwa na jumla ya mabao 36 kwenye Ligi Kuu England na walileta mafanikio ambayo hayajawahi kushuhudiwa pale Stamford Bridge.

### Peter Crouch na Jermaine Defoe

Peter Crouch na Jermaine Defoe walikuwa warithi wa kiti cha enzi cha Quinn na Phillips, waliunda ushirikiano katika vipindi viwili tofauti tangu wadogo, kwani walianza kucheza kwa upatika kule Portsmouth na baadaye Tottenham Hotspur. Wawili hao pia waliungana kwenye majukumu ya kimataifa mara kwa mara, ingawa hakuna aliyepata mafanikio makubwa kwenye timu ya taifa.

### Steven Gerrard na Fernando Torres

Steven Gerrard na Fernando Torres hawakukaa pamoja kwa muda mrefu sana pale Anfield, lakini walitumia muda wao kuwa bega kwa bega. Katika nusu ya mwisho ya kucheza pamoja, wawili hao walitoa ushirikiano mzuri chini ya Rafael Benitez, huku Gerrard mara nyingi akitumika kwa kumlisha pasi nzuri Torres.

Wawili hao nusura watwae taji la kwanza la Ligi Kuu kwa Liverpool kwa kipindi cha miaka 30 katika msimu wa 2008/09.

### Sergio Ramos na Pepe

Sergio Ramos na Pepe walipoingia uwanjani walionekana kama safu ya ulinzi katili zaidi. Si tu kwa sababu walikuwa mabeki wa kati wa kipekee, lakini kutokana na uhodari wao wa kuwazuia washambuliaji wa timu pinzani.

Wawili hao walilinda ngome ya Real Madrid kwa muongo mmoja na kuwasaidia 'Los Blancos' hao kuongeza mataji kwenye kabati lao. Walitwaa mataji matatu ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, mataji ya LaLiga na mawili ya Klabu Bingwa Dunia.

### Giorgio Chiellini na Leonardo Bonucci

Ukizungumza kuhusu vitendo vya kujihami vya kutisha na vya kupambana kwa mabeki wa kati, huwezi kuacha kuwazungumzia Giorgio Chiellini na Leonardo Bonucci. Hawa walirithi mikoba ya Maldini na Baresi kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya Italia na walifurahia mafanikio ya kuvutia katika Klabu ya Juventus.

Ushindi wa Italia wa Kombe la Euro 2020 kwa kiasi kikubwa ulichangiwa na uimara wa safu ya ulinzi ya wawili hao.

### Daniel Sturridge na Luis Suarez

Muda wa Luis Suarez na Daniel Sturridge pamoja ulikuwa mfupi, lakini mtamu sana. Wawili hao kwa haraka waliunda ushirikiano mzuri wakati wakiongoza safu ya Liverpool, wakitoa kampeni zao zilizozaa matunda msimu wa 2013/14 huku Wekundu wakikaribia kunyakua taji la kwanza la Ligi Kuu England kwa kipindi cha miaka 30.

Walifunga mabao 52 kwa pamoja kwenye ligi katika msimu mzima na wote walitoa matokeo mazuri kwenye hatua kubwa zaidi. Suarez aling'ara sana, lakini mguu wa kushoto wa Sturridge ulicheza zaidi ya jukumu lake katika ushirikiano huo wa kuvutia.

### Arjen Robben na Franck Ribery

Arjen Robben na Franck Ribery hawa walikuwa ni kama hiridhi ya Bayern Munich. Wakicheza pembeni, hawakutumia muda mwingi wakiwa karibu sana uwanjani, lakini walikuwa wawili walioleta mafanikio makubwa pale Bayern.

Walitawala soka la Ujerumani walikuwa maarufu kwa kukata ndani na kulenga goli, wakifunga idadi kubwa katika kikosi cha Bayern.

### Harry Kane na Son Heung-min

Hakuna kombinesheni ambayo ilikuwa bora kwenye Ligi Kuu England kama Harry Kane na Son Heung-min walivyofanya pale Tottenham Hotspur. Mwingereza huyo mahiri na Mkorea Kusini asiyechoka walifunga mabao 47 katika maisha yao waliyokaa pamoja pale Spurs.

Uwezo wa Kane wa kufunga, kushikilia mpira juu na kucheza pamoja katika nafasi ya kina zaidi ulimruhusu Son kustawi kwenye ubavu wa kushoto, huku wawili hao wakipata hadhi yao kama magwiji wa Tottenham.

Kwa bahati mbaya kwa Son, kuhama kwa Kane kwenda Bayern kulimaliza urafiki wao wa uwanjani.

## Nukuu

"Sitaki kukaa mahali nikihisi kama mimi ni shida, sitaki kubaki hapa kwa sababu tu mkataba upo, Mwenyekiti wangu anajua. Nilimwambia nipe nafasi nijaribu kurejea', na hasa kila mtu anaporudi [kutoka kuuguza majeraha] na kuona kitakachotokea," **Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola.**



"Bukayo Saka na Martin Odegaard wanamuunganiko mzuri wakati fulani na walionekana kama timu ambayo tumeiona kwa miaka kadhaa iliyopita. Inaonesha kila mtu kile Odegaard anafanya kwa timu hii - anaiunganisha pamoja. Yeye ndiye gundi katika timu. Ni furaha kabisa kutazama na unaona jinsi wanavyokuwa naye vema," **Mchambuzi wa soka, Jamie Redknapp, baada ya Arsenal kushinda mabao 5-2 dhidi ya West Ham United juzi, Jumamosi.**



"Harry alisema kuwa haikuwa mbaya lakini itabidi afanyiwe uchunguzi, itakapofika Jumanne itakuwa ngumu sana - sijui wachezaji wengi ambao wanaweza kupona haraka, lakini tutaona. Mabao yaliyofungwa na Harry Kane hayawezi kupatiwa mbadala, lakini tuna imani na kikosi kizima," **Kocha wa Bayern Munich, Vincent Kompany, baada ya Harry Kane kuumia juzi, Jumamosi wakati wakitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Borussia Dortmund**





# TETESI 10 ZILIZOSHIKA KASI DIRISHA DOGO LA USAJILI

BAYO

Straika wa Kimataifa wa Uganda, Fahad Bayo, anayetajwa kufuatiliwa kwa karibu na viongozi wa Yanga, ili kumsajili kipindi cha dirisha dogo la usajili. **PICHA: MTANDAO**

**Na Adam Fungamwangwo**

KATIKATI ya mwezi huu, Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), linatarajia kufungua dirisha dogo la usajili kwa ajili ya timu za Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi ya Championship, Ligi ya Wanawake na 'First League' kwa ajili ya kuboresha vikosi vyao.

**Hapa nchini Simba moja kati ya timu chache ambazo tayari zimeshawapa wachezaji mikataba na kusubiriwa, tarehe, ikiwa imefanya hivyo kwa winga Elie Mpanzu.**

Hata hivyo, Simba wenyewe na timu zingine kwa sasa bado zipo kwenye pilikapilika ya kusaka wachezaji wengine kwa ajili ya kuziba mapengo ambayo makocha wanaona wanapaswa kuyajaza, baada ya nusu msimu wa ligi na kuona mapungufu kadhaa.

Tayari zipo tetesi za viongozi wa klabu kuhaha huko na huko kusaka na kupata wachezaji ambao wanataka kuwavuta kwenye vikosi vyao.

Katika makala haya, tukuletea tetesi 10 za wachezaji kutoka ndani na nje ya nchi ambao wanatarajiwa kujiunga na klabu za Ligi Kuu Bara baada ya dirisha hilo kufunguliwa, Desemba 15, mwaka huu, kabla ya Januari 16, mwakani.

**1# Denis Lukumbi - Simba**

Klabu ya Simba imetajwa kuwa ipo mawindoni kusaka saini ya straika wa kimataifa wa Uganda, Dinis Lukumbi.

Imedaiwa kuwa viongozi wa Simba wanazungumza na Klabu ya Kitara FC ya Ligi Kuu nchini humo ambayo mchezaji huyo anaichezea kwa sasa.

Straika huyo aliyejiunga na timu hiyo msimu uliopita akitokea Booma FC, alimaliza msimu akishika nafasi ya pili kwenye upachikaji mabao akifumania nyavu mara 14, chini ya Muhhamad Shaban wa KCCA ambaye ajaa kambani mara 17. Simba inataka kuongeza nguvu kwenye safu yao ya ushambuliaji kipindi cha dirisha dogo ili kuwapa changamoto Steven Mukwala na Leonel Ateba, ambapo inatajwa Lukumbi anatarajiwa kupewa mkataba wa mwaka mmoja kwanza.

**2# Fahad Bayo - Yanga**

Kama ilivyo kwa Simba, mabosi wa Yanga nao wamekimbilia nchini Uganda kusaka straika, ambapo tetesi zinasema wameangukia kwa mchezaji wa Timu ya Taifa, The Cranes, Fahad Bayo.

Mchezaji huyo ambaye kwa sasa anaichezea Klabu ya MFK Vyskov ya Czech, anakaribia kumaliza mkataba wake msimu huu, huku akiwa na uwezo wa kuuvunja ili kuhamia Jangwani kama watafikia makubaliano.

Bayo mwenye miaka 26, anatajwa kuwa muarobaini wa mastraika wa Yanga kukosa mabao msimu huu, huku viwango vya Prince Dube na Jean Baleke bado vikizidi kutia shaka.

**3# Selemani Mwalimu - Simba**

Inaonekana Simba bado wamepania kushusha mastraika, kwani tetesi zinasema wamepiga hodi Klabu ya Fountain Gate kutaka huduma ya kinara wa mabao kwenye Ligi Kuu ya Zanzibar msimu uliopita akiwa na timu ya KVZ, Selemani Mwalimu, na kinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa akiwa na mabao sita, Selemani Mwalimu.

Viongozi wa Simba wameonekana kuvutiwa na umbile lake, nguvu, uwezo wa kujiweka kwenye nafasi ya kufunga na kikubwa zaidi, uwezo wa kutumia nafasi chache zinazopatikana kuwa mabao.

Viongozi wa Fountain Gate, hivi karibuni walikaririwa wakisema hawana matatizo kumuuza kijana wao, mradi tu dau wanalotaka lifikiwe.

**4# Lameck Lawi - Yanga**

Klabu ya Yanga inamhitaji kwa udi na uvumba, beki Lameck Lawi kwa ajili ya kuboresha eneo la ulinzi, hasa beki wa kati ambalo linaonekana limeanza kuyumba.

Mchezaji huyo wa Coastal Union, nusura msimu uliopita ajiunge na Simba, kama klabu yake isingekomaa na kukata katakata, ikiwamo kumpeleka nje ya nchi kufanya majaribio yalifyofeli.

Yanga ina matumaini ya kumchukua beki huyo kipindi cha dirisha dogo, inaonekana kuwa viongozi wa timu hizo mbili wana maelewano, kwani waliwahi kuwauzia Bakari Mwamnyeto, pia Coastal iliwahi kupewa kwa mkopo wachezaji, Gustavo Saimon, Yusuph Athumani na Crispin Ngushi.

**5# Ladack Chasambi - Singida Black Stars**

Tetesi zinasema Klabu ya Singida Black Stars, imetuma maombi kwenye Simba kwa ajili ya kumsajili winga, Ladack Chasambi, au kupewa kwa mkopo.

Mabosi wa timu hiyo wameona kuwa kijana huyo atawasaidia kwenye kampeni yao ya kutaka kucheza mechi za kimataifa msimu ujao, kwani wanajua kuwa kwenye kikosi cha 'Wekundu wa Msimbazi', kuna ingizo jipya la Elie Mpanzu, hivyo kutakuwa na patashika ya kuwania namba.

**6# Deus Kaseke - Pamba Jiji**

Winga wa zamani wa Yanga, Mbeya City na Singida Big Stars, Deus Kaseke, anatarajia kujiunga na Pamba Jiji kipindi cha dirisha dogo kama mchezaji huru.

Habari kutoka ndani ya klabu hizo zinasema, mchezaji huyo ameshasaini mkataba na kuanza mazoezi na timu hiyo, kinachosubiriwa ni kupulizwa tu kipenga cha dirisha dogo kama ilivyo kwa Mpanzu na Simba.

**7# Abdelhay El Forsy - Simba**

Tetesi zinasema Simba ipo kwenye mazungumzo na Klabu ya Renaissance ya Morocco ili kukamilisha uhamisho wa mkopo wa mwaka mmoja wa kiungo mshambuliaji huyo.

El Forsy alisajiliwa mwaka 2022 na Raja Casablanca kisha akapelekwa Renaissance kwa mkopo wa mwaka mmoja, lakini kwa sasa wamemsajili moja kwa moja.

Simba wanatarajia kumsajili kwa mkopo kwa msimu mmoja endapo kila kitu kitaenda vizuri.

**8# Kelvin Yondani - Pamba Jiji**

Klabu ya Pamba Jiji, imetajwa kukamilisha usajili wa beki wa kati, Kelvin Yondani, akiwa kama mchezaji huru.

Taarifa zinasema amesaini mkataba wa mwaka mmoja na atajiunga na timu hiyo kipindi cha dirisha dogo la usajili. Yondani, ambaye kwa sasa hana timu baada ya kuachana na Geita Gold, aliwahi kuzichezea Klabu za Simba, Yanga.

**9# Yusuph Athumani - Fountain Gate**

Winga wa zamani wa Yanga, Yusuph Athumani, anatajiwa kusajiliwa na Fountain Gate, ambapo kinachosubiriwa sasa ni ufunguzi wa dirisha dogo la usajili ili atambulishwe. Klabu hiyo imemsajili akiwa mchezaji huru.

**10# Kibwana Shomari - KMC**

Taarifa zinasema kuwa Klabu ya KMC, imepanga kumsajili beki wa pembeni wa Yanga, Kibwana Shomari, kwa mkopo kutoka Yanga.

Beki huyo anayemudu nafasi zote za pembeni, amekuwa hapati nafasi ya kucheza kwenye kikosi cha Yanga, licha ya kusaini mkataba utakaombakisha hadi 2026.

KMC ina uhakika kuwa inaweza kumnasa kwani mabosi wa Yanga watataka aende ili apate nafasi ya kucheza kwa ajili ya kuboresha kiwango chake, ambapo kama kitakuwa cha juu, basi watamrejesha baada ya ligi msimu huu kumalizika.

**JE, WAJUA?**




ARSENAL haijapoteza mchezo wowote wa Ligi Kuu England ambao Martin Odegaard amecheza tangu Aprili mwaka huu - lakini inafahamika kutokana na baadhi ya takwimu muhimu kwamba ingawa Bukayo Saka amecheza mara mbili ya dakika za Odegaard, ana zaidi ya mara mbili ya namba ya Mnorway huyo katika vipimo kadhaa muhimu. Katika dakika 499 alizocheza Odegaard mechi za Ligi Kuu, amefunga bao moja na 'asisti' mbili wakati Saka dakika 981 amefunga mabao matano na asisti 10.



## Ushahidi chanzo kesi za ukatili kijinsia kukwama

Na Elizabeth Zaya

WAKILI wa Serikali Mkuu, Renatus Mkude, amekili kuwa sababu inayokwamisha mapambano dhidi ya kesi zinazohusu mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia ni kukosekana kwa ushahidi zinapofika mahakamani.

Alisema hayo mwishoni mwa wiki kwenye mjadala wa kitaifa wa kuangalia hali ya ukatili wa kijinsia Tanzania katika Siku ya Kimataifa ya Wanawake Watetezi wa Haki za Binadamu ulioandaliwa na Shirika la Wanawake Katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika(WiLDAF) pamoja na Mtandao wa Kupinga Ukatili Tanzania(MKUKI).

Mkude alisema sheria imetamka bayana kwamba ili uthibitishe kosa husika ni lazima uwe na ushahidi lakini bahati mbaya kesi nyingi za ukatili zimekuwa zikikosa ushahidi wa kutosha wa kuthibitisha na hivyo kukwamisha mapambano katika eneo hilo.

"Ofisi yetu ya mashtaka jukumu lake kubwa ni kuendesha mashtaka kwa niaba ya serikali na jukumu la kuthibitisha mashtaka liko upande wa mashtaka, kwa hiyo kuna wakati linatokea tukio la kweli na tunasikitika huyu mtu amebakwa, ameuawa, lakini ushahidi unakosekana kuthibitisha hilo.

"Hapo ndiyo inapokuja kwamba katika kupinga ukatili wa kijinsia, ukamataji na uendeshaji mashtaka siyo njia pekee ya kupinga au ya kuondokana na tatizo la ukatili wa kijinsia, tunapaswa kujitahidi kuwa na ushahidi.Tunweza kuwa na sheria nzuri lakini kama hakuna ushahidi tunaweza kukwama,"alisema Mkude.

Mkurugenzi wa WiLDAF, Anna Kulaya, alisema katika kuangalia hali ya ukatili, mwaka jana na mwaka huu walibaini kwamba kesi nyingi ambazo zimekuwa zikikwama mahakamani ni za eneo hilo la ukatili wa kijinsia.

"Tumebaini kwamba kesi nyingi zinazoripotiwa ni za ukatili wa kingono hususani ubakaji ambazo ni asilimia 54 ya kesi zote za ukatili wa kijinsia zinazoripotiwa, zikifuatiwa na za ulawiti. Hii haimanishi kwamba aina nyingine za ukatili hazifanyiki lakini kimsingi watu wameripoti zaidi ubakaji," alisema Kulaya.

Aliongeza: "Tulibaini kwamba Jeshi la Polisi limefanya kazi kubwa kwa kufikisha kesi nyingi mahakamani lakini zikifika huko zinakwama na kuna mlundikano mkubwa mpaka sasa wa kesi hizo, kwa hiyo bado kidogo kuna shida. Kwa hiyo tunajadili kwamba tunakwama wapi, mifumo yetu ya upatikanaji haki inashida gani."

Aidha, alitoa wito kwa mahakama kujitahidi katika kutoa kipaumbele kwa kesi hizo ili kusaidia katika mapambano yake kwa kuwa vinaathiri kundi kubwa katika jamii.

# Miaka saba, mimba za utotoni zapungua kwa 17%

Na Renatha Msungu, DODOMA

MATUKIO ya mimba za utotoni kwa wasichana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 19 mkoani Dodoma yamepungua kutoka asilimia 39 kwa mwaka 2015/16 hadi asilimia 22.7 kwa mwaka 2022.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule alitoa takwimu hizo jana wakati wa hafla ya kufunga mradi wa connect uliotekelezwa ndani ya miaka mitano na Shirika lisilo la kiserikali la Save the Children kwenye Wilaya ya Bahi na Kongwa.

Alisema mikakati iliyowekwa na mkoa huo imeleta tija na kufikia kiwango hicho na kwamba wataendelea kutokomeza matukio hayo kwa kushirikiana na wadau.

**"Takwimu za kitaifa zinaonyesha kuwa asilimia 27 ya wasichana wa umri kati ya miaka 15 hadi 19 tayari wamepata ujauzito na kwa Mkoa wa Dodoma, mwaka 2015/16 ...**

"Takwimu za kitaifa zinaonyesha kuwa asilimia 27 ya wasichana wa umri kati ya miaka 15 hadi 19 tayari wamepata ujauzito na kwa Mkoa wa Dodoma, mwaka 2015/16 ilikuwa ni asilimia 39 kwenye utafiti wa kitaifa, kiwango ambacho ni kikubwa zaidi ya kiwango cha kitaifa na ndiyo maana mkoa tuliamua kutekeleza mikakati ya kupunguza changamoto hii," alisema Senyamule.

Kaimu Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Save the Children, Anatoli Rugaimukamu alisema mafanikio yaliyopatikana kwenye mradi huo ni pamoja na kuwajengea uwezo wahudumu wa afya ngazi ya jamii 100 ambao wamefanikiwa kuwafikia zaidi ya kina mama 5,776. Alisema wametoa mafunzo kazini kwa wahudumu 253 kwenye vituo vya afya 31 katika Wilaya ya Bahi na Kongwa mkoani hapa, lengo ikiwa ni kuhakikisha akinamama wanapata elimu juu ya njia za kisasa za uzazi wa mpango baada ya kujifungua.

Aidha, alisema wahudumu hao wa ngazi ya jamii wataendelea kutoa elimu kwa kinamama kuhusu umuhimu wa kutumia njia za kisasa za uzazi wa mpango, ambazo zitawasaidia kuendelea na shughuli mbalimbali ikiwamo ujasiriamali wanaofanya ili kujiinua kiuchumi.

Mkazi wa Wilaya ya Kongwa, Devotha Charles, alisema mradi huo umesaidia kinamama wengi vijana kutambua umuhimu wa kutumia njia za uzazi wa mpango.




Naibu Waziri wa Ujenzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya (kulia), akipata maelezo kuhusu vifaa vinavyotumiwa na mafundi kupima umeme wa Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA), alipotembelea maonesho ya makandarasi, jijini Dodoma, mwishoni wa wiki. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# RC acharuka usajili wakulima ukizorota, atoa agizo

Na Thobias Mwanakatwe, SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, ametoa wiki mbili kwa wakuu wa idara ya kilimo wa halmashauri za mkoani humo kuhakikisha wanasajili wakulima kwa asilimia 85 kwa ajili ya kupata pembejeo za kilimo.

Amesema endapo atakwepo yeyote atakayeshindwa kufikia lengo hilo aandike barua ya kuacha kazi.

Alitoa agizo hilo wakati akizungumza kwenye kikao cha wadau wa kilimo baada ya kupewa taarifa kwa kila halmashauri kuhusu utekelezaji wa shughuli za kilimo.

Alisema bado kiwango cha usajili wakulima kwenye daftari la wakulima kipo chini ukilinganisha na lengo lililowekwa na mkoa.

"Acheni uvivu na kuniletea maneno ya uongo mimi sitawaacha nataka kuona hadi kufika mwisho wa msimu wa kilimo nani ananikwamisha na pia kiwango cha usajili wakulima kifikie asilimia 85 na utashindwa kufanya hivi Andika barua ya kuacha kazi Desemba 15, 2024," alisema.

Dendego alisema suala la kilimo linapaswa kupewa kipaumbele namba moja, hivyo hatakubali kuona wapo baadhi ya maofisa kilimo wanakwamisha jitihada za serikali katika kuinua sekta ya kilimo mkoani humo.

Aidha, alimwagiza Mkuu wa Idara ya Kilimo Mifugo na Uvivu Wilaya ya Iramba, Marietha Kasongo, kuhakikisha analipa deni la Sh.milioni 35 wanazodaiwa na Kiwanda cha mbolea cha Intracom kilichopo mkoani Dodoma.

Katibu Tawala Msaidizi sehemu ya Uchumi na Uzalishaji, Stanslaus Choaji, alisema namna bora ya kuwafanya wakulima wasisononeke na Mkoa wa Singida kuonekana kuwa wa mwisho ni kuongeza msukumo katika suala la kilimo na kuongeza uzalishaji.

Chaoji alisema kutokana na Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) mvua mwaka huu zitakuwa chini ya kiwango hivyo wakuu wa idara ya kilimo wahakikishe wakulima wanafikishiwa pembejeo haraka.





# Wakulima wa chai kicheko, masoko yakipatikana

**Na Halfani Chusi**

BODI ya Chai Tanzania imeanza kurejesha masoko ya chai yaliyopotea, lengo likiwa ni kukabiliana na matatizo wanayokumbana nayo wakulima.

Kaimu Mkurugenzi wa bodi hiyo, Beatrice Banzi alisema hayo jijini Dar es Salaam baada ya kutembelewa na Mkurugenzi wa Kampuni ya Kimataifa ya Chai Omani, Khalfan Abdullah.

Alisema zamani walikuwa wananunua chai hapa nchini lakini baadaye waliacha kutokana na sababu mbalimbali.

Alisema katika mazungumzo yao ya kuwarejesha upya wameahidi kununua tani 100 za chai kwa mwezi na kwa mwaka tani 1,200.

Beatrice alisema hatua hiyo itasaidia kumaliza kilio cha wakulima wa chai Mponde wilayani Lushoto mkoani Tanga cha kukosa soko.

"Wamesema Desemba 15 mwezi ujao wataanza kununua chai, nimepokea kwa sura ya furaha ahadi yao, tumeanza kufungua njia kwa masoko yaliyofungwa na kupata mengine mapya.

"Hili ndio lengo la Bodi ya Chai, Wizara ya Kilimo, na serikali kwa ujumla ni kuona tatizo la soko la chai nchini linafikia ukomo. Wakulima wasikate tamaa bodi ya chai ipo inaendelea kutafuta masoko ndani na nje ya nchi, ili kuwasaidia kuuza mazao yao kirahisi" alisema Beatrice

**"Hili ndio lengo la Bodi ya Chai, Wizara ya Kilimo, na serikali kwa ujumla ni kuona tatizo la soko la chai nchini linafikia ukomo. Wakulima wasikate tamaa bodi ya chai ipo inaendelea kutafuta masoko..."**

Alisema mbali na kuwarejesha wanunuzi hao kutoka Oman wameanza kurejesha la soko la Sudan akikumbushia kuwa siku chache zilizopita walikwenda ubalozi wa nchi hiyo kwa ajili ya kuangalia namna ya kutanua soko la bidhaa hiyo mahali huko.

Aliongeza kuwa serikali tayari imeagiza mashine kwa ajili ya kujenga viwanda vya kuchakata chai, akisema hatua hiyo itasaidia kupunguza changamoto ya soko kwa wakulima.

Aidha, aliwataka wakuu wa kampuni, mashirika na vyama vinavyojihusisha na masuala ya chai kuendelea kuwatembelea wakulima wa chai ili kusikiliza na kutatua kero zao.

Ofisa Masoko wa bodi hiyo, Selemani Chilo alisema kufufuka kwa soko la chai Oman kutaisadia Tanzaia kuingiza Dola za Marekani milioni 1.5 kwa mwaka (Sh. bilioni 3.9).



Mkuu wa Chuo Kikuu Mzumbe, Dk. Mohamed Shein (katikati), akiwa ameongozana na baadhi ya viongozi wa chuo hicho, kwenye maandamano ya kitaaluma wakati wa mahafali ya 23 ya Chuo hicho Ndaki ya Mbeya, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wahitimu vyuo vikuu watakiwa kutochagua kazi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAHITIMU wa vyuo vikuu wametakiwa kuendelea kujifunza mambo mapya ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia duniani ambayo yatawasaidia kujiletea maendeleo na taifa.

Pia, wametakiwa kuacha kuchagua kazi na badala yake wafanye kazi yoyote halali ya kuwaingizia kipato, zikiwemo kazi za kujiajiri na kuacha kulalamikia ukosefu wa ajira.

Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, Dk. Ally Shein alitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki kwenye mahafali ya 23 ya chuo hicho ndaki ya Mbeya ambapo aliwataka wasibweteke baada ya kuhitimu shahada zao.

Alisema kuna baadhi ya wahitimu wa vyuo vikuu wamekuwa wakikosa ajira kutokana na kutojituma kwa sababu ya kuwa na fikra potofu za kutegemea ajira ya serikalini pekee. "Kwa sasa dunia imebadilika, dunia ilivyo sasa ni tofauti na itakavyokuwa mwaka 2050, kutakuwa na mabadiliko mengi ya teknolojia na baadhi yenu mtafika huko, kwahiyo ili muendane na mabadiliko hayo hakikisheni mnajiendeleza kwa kusoma," alisema Dk. Shein.

Dk. Shein alisema kwa sasa serikali inawategemea wasomi wa vyuo vikuu kusaidia kwenye maeneo mbalimbali ya maendeleo.

Makamu Mkuu wa Chuo cha Mzumbe, Prof. William Mwegoha alisema chuo hicho pamoja na maendeleo mbalimbali ambayo kimepata lakini kinakabiliwa na uhaba wa mabweni kwa ajili ya wanafunzi, hali ambayo inasababisha wengi wao kuishi nje ya chuo.

Alisema kwa sasa uongozi wa chuo hicho kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, wameanzisha harambee kwa ajili ya kuanza ujenzi wa hosteli za wanafunzi hasa kwa ajili ya wanafunzi wa kike ambao ndiyo wanakabiliwa na matatizo mengi.

Alisema ili kukamilisha ujenzi wa bweni hilo wanahitaji zaidi ya Sh. bilioni tano lakini mpaka sasa wamekusanya Sh. milioni 90 pekee hali ambayo inachelewesha kuanza kwa mradi huo.

Alisema fedha hizo zimechangwa na wadau mbalimbali wakiwemo wanafunzi waliohitimu chuo hicho miaka ya nyuma pamoja wadau wengine wa maendeleo.

"Tulipokuwa kwenye mahafari kama haya kule Morogoro Rais Samia Suluhu Hassan aligusiwa na tatizo hili la uhaba wa mabweni na alituahidi kutushika mkono, lakini tunaomba wadau waendelee kujitoa ili tukamilishe mradi wetu," alisema Prof Mwegoha.

Alisema chuo hicho kina wanafunzi wengi lakini wanaokaa hosteli za chuoni ni wachache na hivyo kusababisha idadi kubwa kuishi nje ya chuo hasa kwenye makazi ya watu binafsi ambako wanakumbana na matatizo mbalimbali.

Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi wa chuo hicho, Prof. Saida yahya aliipongeza serikali kwa kuanza kubadili mitaala hasa kwa kaanza kuimarisha mafunzo ya vitendo akidai kuwa mitaala hiyo itasaidia kupunguza tatizo la ajira.

# DC: Uchaguzi umeisha twendeni shambani tukalime

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa amewataka wananchi wilayani humo kuelekeza nguvu kwenye msimu mpya wa kilimo na kuacha kufikiria siasa kwa maelezo kuwa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa umemalizika.

Alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki wakati akitoa shukrani kwa viongozi wa dini wa madhehebu mbalimbali ofisini kwake.

"Uchaguzi umeisha na sasa mawazo yote wananchi tuelekeze kwenye uzalishaji wa kilimo. Ni msisitizo wetu sisi serikali, na niwaombe viongozi wa dini tuangalie kitu gani kinafuata baada ya huu uchaguzi kwamba tuendelee na shughuli zetu za kawaida," alisema Kissa.

Alisema Mungu amesaidia uchaguzi umeisha watu wakiwa imara na wamoja bila ya kutokea matukio ya kuhatarisha amani.

"Njombe ipo salama na amani, Mungu amekuwa ni mwema lakini ni kwa sababu viongozi wa dini na wananchi tuliweza kuungana kwa pamoja na nyinyi wenzetu mliweza kumuomba Mungu na sisi waumini wenu tulisikiliza maonyo ambayo mliyatoa," alisema Kissa.

Baadhi ya viongozi wa dini walisema uchaguzi ulifanyika kwa kuzingatia demokrasia na haki, huku kampeni zikiendeshwa kistarabu hali iliyosaidia kutokuwa na uvunjifu wa amani.

Wakizungumza katika kikao hicho, Askofu Msaidizi wa Jimbo la Njombe wa Kanisa la EAGT, Ibrahimu Mtonyole alisema amani yote iliyopatikana katika kipindi chote cha uchaguzi ni kutokana na maombi yaliyofanywa na viongozi wa dini usiku na mchana.

"Lakini pia tukuhakikishie sisi kama wachungaji na maaskofu tuko pamoja na serikali kuhakikisha kwamba tunaombea amani ili nchi yetu iendelee kuwa na amani na utulivu kama ulivyo uchaguzi katika sehemu nyingine tumesikia mauaji lakini sio Njombe," alisema Mtonyole.

Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Ushirika wa Njombe Mjini, Nelson Godiwe alisema nchi imefanya siasa za kizalendo na wananchi wamechagua kile ambacho wameelewa.

Alitoa wito kwa wananchi kuendelea na ndoto ambazo wanazo kwa taifa na kwa familia zao ili kuweza kufikia hatima kwa kuwa kwenye uchaguzi lazima kukubali kwamba kuna mmoja atatangulia mbele na wengine watafuata.

Katibu Tawala Wilaya ya Njombe, Agatha Mhaiki aliwaomba viongozi wa dini kwenda kuwakumbusha wazazi kipindi cha likizo watoto wanaporudi nyumbani kufundishwa maadili.



# Utafiti uingizaji madini ya ujenzi Z'bar wakamilika

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Maji, Nishati na Madini imesema imekamilisha utafiti wa uingizaji wa madini ya ujenzi kutoka Tanzania Bara, kwa lengo la kupunguza matumizi ya madini hayo Zanzibar.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa wizara hiyo, Zawadi Amour Nassor katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, wakati akijibu swali la mwakilishi wa Mwanakwerekwe, Ameir Abdalla Ameir.

Ameir alitaka kujua ni utafiti ngapi zilizofanyika katika kutoa mwelekeo mzima wa upotevu wa mali zisizorejeshwa ikiwa ni pamoja na mchanga, vifusi na mawe.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema utafiti huo ulilenga aina za madini ya ujenzi yanayoweza kuingizwa Zanzibar, maeneo ya upatikanaji, miundombinu ya usambazaji, pamoja na gharama.

Alisema wizara imeanza uhuishaji wa maeneo mbalimbali yaliyochimbwa madini ya ujenzi kwa kupanda miti katika maeneo yaliyochimbwa mchanga na baadhi ya maeneo kujazwa udongo kwa ajili ya matumizi ya kilimo na baadhi ya maeneo yaliyochimbwa vifusi wamepatiwa wajasiriamali na wameyabadilishia matumizi kuwa mabwawa ya samaki.

Aidha, alisema katika uhuishaji huo kuna baadhi ya changamoto zimejitokeza ikiwemo kuibiwa kwa miti hasa ya matunda na maeneo hayo kutumika kama malisho ya wanyama.

Waziri wa Wizara hiyo, Shaibu Hassan Kaduara akijibu swali la nyongeza lililoulizwa na mwakilishi huyo aliyetaka kujua sababu za kusitisha uchimbaji wa mawe na baadaye kurudisha.

Alisema machimbo ya madini ambayo kwa Zanzibar wanatumia kwenye ujenzi ni mawe ambao uzuiaji wake ulitokana na utafiti zilizofanyika na kubaini uhaba wake.

# Makamu wa Rais azifariji familia 28 zilizoathirika na upepo mkali

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman, amesema kuzuka kwa upepo mkali, vimbunga, matetemeko ya ardhi na mvua zisizotabirika katika maeneo mbalimbali duniani ikiwemo Zanzibar, ni miongoni mwa athari za mabadiliko ya tabianchi.

Othman ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama ACT- Wazalendo Taifa aliyasema hayo katika Wilaya ya Micheweni Kaskazini Pemba, alipofika kuzifariji familia 28 zilizoathirika kwa upepo uliozuka Novemba 22 na kuleta athari katika Kijiji cha Mgogoni.

Miongoni mwa athari zilizosababishwa na upepo huo ni baadhi ya nyumba 14 kuharibika, mazao ya Chakula na biashara pamoja na vyombo vya usafiri vya wananchi kuangukiwa na miti.

Othman alisema serikali itaendelea kuwa pamoja nao kusaidia jitihada za pamoja katika kuhakikisha kwamba maisha ya wananchi hao yanarudi katika hali ya kawaida.

Alisema mamlaka zinazohusika na usimamizi wa masuala ya maafa zinaendelea na kazi ya kufanya tathmini ya madhara yaliyotokana na upepo huo, ili kuhakikisha kunapatikana taarifa sahihi za kiwango cha madhara na kuchukua hatua zinazostahiki kwa mujibu wa sheria ya kusimamia masuala ya maafa Zanzibar.

**Hivyo, aliwataka wananchi kuendelea kumshukuru Mungu hasa kwa kuwa Zanzibar kijografia haipo katika eneo hatarishi kama zilivyo nchi nyingine duniani.**

Alisema katika baadhi ya nchi mbalimbali duniani zenye visiwa kama Zanzibar kwa kijiografia zimekuwa zikikumbana na maafa ya aina hiyo takribani kila mwaka.

Hivyo, aliwataka wananchi kuendelea kumshukuru Mungu hasa kwa kuwa Zanzibar kijografia haipo katika eneo hatarishi kama zilivyo nchi nyingine duniani.

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Salama Mbarouk Khatib, alisema tayari serikali ya mkoa huo imeanza kuchukua hatua za awali kuwasaidia wananchi hao wakati ikendelea kusubiri tathimini kamili ya athari.

Naye Mkurugenzi wa Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar, Makame Khatib Makame, alisema serikali kupitia ofisi hiyo inaendea kufanya tathimini rasmi ili kupata taarifa kamili na sahihi na kutambua kiwango cha athari zilizotokana na maafa hayo na hatua stahili ziweze kuchukuliwa kwa mujibu wa sheria.

Alisema kwamba upepo huo uliozuka majira ya saa nne asubuhi ya Novemba 22, mwaka huu ulikuwa mkali na kwamba athari kwa wananchi hao pia ilikuwa kubwa.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harous Said Suleiman aliwataka wananchi hao kuwa wastahimilivu na kuendelea kuonesha upendo na umoja miongoni mwao kwa kusaidiana.



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, akizungumza na baadhi ya wananchi wa kijiji cha Mgogoni, wilaya ya Micheweni Pemba, juzi, alipofanya ziara ya kuwafariji baada ya kupatwa na maafa ya upepo mkali uliozuka Novemba 22 mwaka huu na kuharibu nyumba. **PICHA: OMKRZ**

# Ujenzi shule nne za ghorofa Unguja waiva

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla amesema uwekaji wa mawe ya msingi katika shule nne za sekondari ni hatua muhimu ya kuweka mazingira bora kwa walimu na wanafunzi katika kujifunza na kufundishia.

Aliyasema hayo katika hafla ya uwekaji wa mawe ya msingi katika shule nne za ghorofa zinazojengwa katika Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema ujenzi wa shule hizo una lengo la kuleta ufanisi na utendaji kazi katika sekta ya elimu, ikiwemo kuwawezesha wanafunzi wote wa Zanzibar kuingia kwa mkondo mmoja wa asubuhi pekee jambo litakalosaidia kuongezeka kwa kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi hao.

Alisema serikali imepanga kuimarisha miundonbinu ya elimu ili wanafunzi wasome katika mazingira rafiki ya kujifunzia pamoja na walimu kufundisha wakiwa na nyenzo zote muhimu.

Alisema Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi amefanya kazi kubwa ya ujenzi wa miradi ya maendeleo Zanzibar ambapo kuelekea shamra shamra za sherehe za Mapinduzi zaidi ya miradi 150 itafunguliwa ambayo itasukuma zaidi kasi ya maendeleo nchini.

Hivyo, aliwataka wananchi kuwa tayari kupisha ujenzi wa miradi ya maendeleo kwa maslahi ya taifa.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Mohamed Mussa alisema miradi ya elimu imegusa maeneo yote ya Zanzibar ikijumuisha ujenzi wa shule za ghorofa, shule za chini, ujenzi wa madarasa mapya na ukarabati wa madarasa yaliyochakaa.

Lela alisema serikali imepanga kuongeza bajeti ya Wizara ya Elimu itakayotumika katika kuendeleza miundombinu na kukuza kiwango cha elimu Zanzibar.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Khamis Abdulla Said alisema shule zilizowekewa mawe ya msingi zitakapokamilika na kufunguliwa zitakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi zaidi ya 6,000 kwa wakati kwa uwiano wa wanafunzi 45 kwa kila darasa.

Khamis alisema ujenzi wa shule hizo na nyingine zinazoendelea kujengwa Unguja na Pemba zina lengo la kupunguza changamoto ya msongamano wa wanafunzi madarasani.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(LAND DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**
**LAND APPEAL NO. 27712 OF 2024**
**ANIPHER CHARLES ............APPELLANT**
**VERSUS**
**CHRISTOPHER JOSEPHAT MRAMBA &**
**ANOTHER ............RESPONDENTS**

**TO,**
**HAPPINESS DADSON GAMA**

WHEREAS: The above named APPELLANT has institute the MEMORANDUM OF APPEAL against you, you are hereby summoned to appear in this court in person or by advocate or authorized Agent on 11th day of DECEMBER 2024 at 10:00 PM for MENTION Before Hon. N.E.M MANDIA, Judge to answer the said APPEAL and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to reply in support of your reply.

**TAKE NOTICE** that in default of your appearance on that day, the said matter will be heard and determined in your absence.

Given under my hand and the seal of this court this 26th day of NOVEMBER, 2024

DEPUTY REGISTRAR

---


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KILOMBERO**
**Kituo cha MKAMBA Mkoa wa MOROGORO**
**Shauri la Ndoa Na.14/2024**
**Jina la Mdai: ERASTO AMOSI MTENDO**
**Jina la Mdaiwa: FADHIRA REMIUS**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za utaratibu wa Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa FADHIRA REMIUS**
**Kwakuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba (NAKUDAI TALAKA KWAKUA UMETOLOKA NYUMBANI KWANGU YAPATA MWANA NA NUSU SASA)**

Hivyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya JUMANNE tarehe 10 mwezi 12 mwaka 2024 saa 2:00 Asubuhi/mchana na kwa mujibu wa madai hayo na kwakuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

ANGALIZO: Kama hutohudhuria siku iliyotajea hapo juu na ikathibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 29 Mwezi 11 Mwaka 2024.




---

## KUPOTEA KWA CHETI



**SOSPETER YOHANA AMOS,** Anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha Nne chenye Index namba S.2464/0067 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia shule ya Sekondari Songambele Kilimani Mwaka 2019. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha Polisi.
**TAARIFA YA POLISI: PHQ/DOD/DOD/45327/2024**

---

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA**
**MAHALI DODOMA**
**MAOMBI/MAOMBI MADOGO/RUFAA NA 125 MWAKA 2024**
**LUHAGA CHRISTOPHER..........MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**PETER LAMECK FUKUNYI ...............1st MJIBU MAOMBI**
**HAPPINESS LAIZER..........2nd MJIBU MAOMBI**
**GLOBALGRID SURVEYOR LTD......3rd MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA PETER LAMECK FUKUNYI,**
**HAPPINES LAIZER,**
**GLOBAL GRID SURVEYOR LTD.**

Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 05 Mwezi 12 Mwaka 2024 saa 3:00 Asubuhi mbele ya Mhe KANYERINYERI Mwenyekiti wa Baraza. Hivyo unaamuriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Unatakiwa/Mnatakiwa ufike/mfike wewe mwenyewe/ninyi wenyewe, au Wakili wako/wenu/mwakilishi wako/wenu pasipo kukosa na ulete/mlete utetezi wako/wenu ndani ya siku ishirini na moja (21) toka tarehe ya kupokea kuitwa shaurini.

Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/ Muhuri wa Baraza hii leo tarehe 17 Mwezi 10 Mwaka 2024

.....................................................................
**MWENYEKITI**
**Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya Dodoma.**


---

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**FEDRICK ANDREA NYALUKE**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI ZAKE ZA PIKIPIKI PAMOJA NA GARI ZENYE USAJILI NAMBA MC 280 CCC, MC 391 CBY, MC 223 BWK. PAMOJA NA GARI YENYE USAJILI T 435 DJX AINA YA SUZUKI VITARA YENYE CHASISI NAMBA JSAETD01V00132339 KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUZIONA KADI HIZI ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI JALADA **PHQ/IRI/IRI/18749/3024, PHQ/MOR/KIL/3517/2023.**

---

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**KALDEN GERARD MALAI** naomba kutangaza kupotelewa na hati yangu ya kusafiria namba **TAE199185** iliyotolewa uhamiaji makao makuu. Yoyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi:**PHQ/DAR/ILA/262751/2024**

---

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**HEBERY INVESTMENT CO. LTD**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI ZA PIKIPIKI ZENYE NAMBA ZA USAJILI MC 188 EBN, MC 107 EFL, MC 835 DYK, MC 201 EKB NA MC 725 ECD ZILIZOTOLEWA NA MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA. KWA YEYOTE ATAKAYEZIONA ANAOMBWA ARIPOTI KWENYE KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHO KARIBU. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/IR/IR/18609/2024**

---

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**HEBERY INVESTMENT CO. LTD**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI ZA PIKIPIKI ZENYE NAMBA ZA USAJILI MC 243 ENN, MC 150 ENN, MC 401 ENM, MC 845 EBP NA MC 260 ENN ZILIZOTOLEWA NA MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA. KWA YEYOTE ATAKAYEZIONA ANAOMBWA ARIPOTI KWENYE KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHO KARIBU. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/IR/IR/18609/2024.**

---

## KUPOTEA KWA CHETI




**PETER NGESI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye **Index No. S0496/0183** Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **JITEGEMEE SECONDARY SCHOOL** mwaka 1999. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/TEM/264016/2024**

---

## KUBADILI JINA



Mimi Sindhu Thulasidas, W/o Thulasee Das T G, raia wa India, mwenye hati ya kusafiria halali ya India M-4237937 na pia mwenye kibali halali cha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania namba RPQB01867923W01 na R/o 212-B, Pocket C-II halali. , Mayur Vihar Phase-III, New Delhi 110096, na kwa sasa ninaishi Dar Es salaam na nimebadilisha jina langu la ukoo kutoka Sindhu Thulasidas hadi Sindhu Thulasee Das kwa madhumuni yote yajayo.




---

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 0677020701**

**E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,**

**WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Trump atishia mataifa yanayochipukia kiuchumi

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS mteule wa Marekani Donald Trump ametishia Umoja wa Mataifa yanayochipukia Kiuchumi (BRICS) yanayoungwa mkono na China na Russia, kwamba endapo yatatengeneza sarafu mpya itakayochukua nafasi ya dola kuu ya Marekani, basi wajiandae kutozwa ushuru wa asilimia 100.

Kiongozi huyo aliyaeleza hayo jana kupitia andiko alilochapisha kwenye mtandao wake wa 'Truth Social' akisema kiwango hicho cha ushuru kitatozwa kwa kila bidhaa itakayoingizwa Marekani na umoja huo ambao Russia ndio mwenyekiti, kipindi chote cha utawala wake.

Alisema wazo kwamba nchi za BRICS zinajaribu kuondoka kwenye dola kuu wakati wao wakisimama na kuangalia, halipo, na kwamba wanahitaji ahadi kutoka kwa nchi hizo kuwa hazitaunda sarafu mpya wala kurudisha nyingine kuchukua nafasi ya dola kuu ya Marekani.

BRICS ambayo awali iliundwa na Brazil, Russia, India, China na Afrika Kusini tangu 2011, mapema mwaka huu, Iran, Saudi Arabia, Umoja wa Falme za Kiarabu, Ethiopia na Misri zilijiunga rasmi ikiwa ni upanuzi wa kwanza katika zaidi ya muongo mmoja.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Afrika Kusini, Naledi Pandor alisema kuwa nchi zingine 34 zimewasilisha onyesho la kutaka kujiunga na kambi ya mataifa makubwa yanayoinukia kiuchumi.

Aidha, ilielezwa kuwa kiongozi wa nchi moja mwanachama, Luiz Lula da Silva wa Brazili, mwaka 2023 alipendekeza kuunda sarafu ya pamoja nchini Amerika Kusini ili kupunguza utegemezi wa dola ya Marekani.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa kutumia sarafu za BRICS na mitandao ya benki nje ya mfumo wa thamani ya dola ya Marekani kunaweza kuruhusu nchi wanachama kama vile Russia, China na Iran kuvuka vikwazo vya Magharibi. Lakini uwezekano wa kupata sarafu mpya huenda ni mdogo kutokana na tofauti za kiuchumi na kijiografia za muungano huo.

Kundi hilo linalopanuka ni la thamani kwa China kwani linatazamia kuunda ushirikiano wa karibu na wahusika wakuu ili kutoa changamoto kwa uongozi wa kimataifa wa Marekani.

Vile vile, ilielezwa kuwa hatua hiyo pia ni neema kwa Russia, ambayo imeepukwa kiuchumi na kidiplomasia na nchi za Magharibi kufuatia uvamizi wake wa 2022 nchini Ukraine. Na kwamba mwaka huu ilichukua uwenyekiti wa kupokezana wa kundi hilo. **CNN**



Kaimu Mkurugenzi Bodi ya Chai Tanzania (TBT), Beatrice Banzi (wa pili kulia) akimsikiliza Mkurugenzi wa Kampuni ya Kimataifa ya Chai Omani, Khalfan Abdullah (wapili kushoto) walipotembelea katika ofisi yao, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kuwashawishi kununua chai inayozalishwa nchini. Kushoto ni mtoto wake, Ruwaiya Alsharji na (kulia) ni Ofisa Masoko wa bodi hiyo, Selemani Chilo. **PICHA: HALFANI CHUSI**

# Mahakama ya Mafisadi yamtia hatiani, yataifisha gari la kifahari

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, maarufu Mahakama ya Mafisadi, imemtia hatiani mfanyabiashara Gastoni Martin na kuamuru gari lake la kifahari aina ya Ford Ranger litaifishwe kuwa mali ya serikali baada ya kukiri kosa la kusababisha hasara na kutakatisha zaidi ya Sh. bilioni moja za Benki ya CRDB.

Hukumu hiyo imetolewa mbele ya Jaji Godfrey Isaya baada ya kuzingatia mkataba alioingia mshtakiwa na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) wa kukiri makosa aliyoshtakiwa kwayo.

Akiwakilisha Jamhuri, Wakili wa Serikali Mwandamizi Habel Kihaka alidai mshtakiwa aliingia mkataba wa kukiri kosa na DPP kwa hiari yake, hivyo aliondolewa mashtaka kuanzia namba moja hadi shtaka la 179 na kubakiwa akikabiliwa na shtaka la 180 na 181.

Wakili Kihaka, akisoma maelezo ya awali ya mashtaka yanayomkabili, alidai mshtakiwa alikuwa na kampuni inayojihusisha na utafiti wa madini inayoitwa Savannah.

Inadaiwa kwa kutumia kampuni hiyo, aliomba benki mkopo wa wafanyakazi 'hewa' 67, lakini Benki ya CRDB ilikubali kuwapa wafanyakazi 35.

Jamhuri wanadai mkopo huo haukulipwa kama makubaliano ya ukopaji yalivyokuwa.

"Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ilifanya uchunguzi na kubaini kampuni ya Savannah ilianzishwa Desemba 20, 1996, ilisajiliwa na kupewa namba 31216," alidai.

Alidai kampuni hiyo ilifungua akaunti ya Dola za Marekani katika Benki ya Stanbic lakini akaunti ilikufa baada ya mwaka 2016 kampuni kurudisha leseni ya utafiti wa madini Wizara ya Madini kutokana na kushindwa kufanya kazi katika eneo ilikoelekezwa.

Inadaiwa kuwa mwaka 2020, mshtakiwa na Regina Massawe waligushi nyaraka mbalimbali za kampuni ya Savannah, ikiwamo leseni, vitambulisho vya wafanyakazi, vitambulisho vya kura kuonesha kampuni inafanya kazi ilhali si kweli.

Wafanyabiashara hao walifungua ofisi ya kampuni katika jengo la ACCACIA, wilayani Kinondoni na kwa kutumia jina la Savannah, mshtakiwa Gastoni alifungua akaunti katika benki ya GT Tawi la Victoria kwa nyaraka za kugushi.

Inadaiwa mshtakiwa alijitambulisha kwa jina la Mariamu Mganga na alikuwa mtia saini pekee katika akaunti hiyo. Pia alikuwa ni Mkuu wa Kitengo cha Fedha huku Regina akiwa Ofisa Rasilimali Watu.

Upande wa Jamhuri unadai wafanyabiashara hao walimwajiri Kenedy Shauri kwa ajili ya kutengeneza logo ya kampuni, mtandao, baruapepe na vitambulisho vya wafanyakazi hewa.

Inadaiwa baada ya kukamilisha, mshtakiwa aliomba mkopo wa wafanyakazi Benki ya CRDB, maofisa wa Benki walitembelea katika ofisi zao wakamkuta mshtakiwa na Regina wakawaelekeza kila mfanyakazi anatakiwa kufungua akaunti binafsi kisha mishahara yao ipitishiwe katika benki hiyo.

"Mshtakiwa, akishirikiana na Regina, walifanikiwa kufungua akaunti 67 za wafanyakazi kwa kutumia nyaraka za kugushi na Agosti 26 na Novemba 27 mwaka 2020, mshtakiwa aliwasilisha maombi ya mkopo CRDB.

"Kati ya maombi ya mkopo kwa wafanyakazi 67, CRDB walikubali kuwapa mkopo wafanyakazi 35 wenye jumla ya Sh. 1,569,600,000.

"Wafanyakazi hewa baada ya kupata mkopo, walitoa kiasi cha fedha na kumkabidhi mshtakiwa na Regina, kiasi kilichobakia katika akaunti hizo kilitolewa na mshtakiwa kwa kutumia kadi ya ATM.

"Mshtakiwa alifanikiwa kutoa fedha katika akaunti 32 kati ya 35 za wafanyakazi hewa. Jumla ya Sh. 1,439,600,000 zilizowekwa Desemba 21 mwaka 2020 zilitolewa kwa haraka," alidai Wakili Kihaka.

Inadaiwa Benki ya CRDB ilipobaini kuna wizi, ilizifunga akaunti zote wakafanikiwa kupata Sh. 6,805,538.82 zilizobakia katika akaunti 32 na jumla ya Sh. 130,000,000 zilikuwa katika akaunti tatu, hivyo kusababisha benki kupata hasara ya Sh. 1,398,535,421.25.

Julai 20, 2020 na Novemba 26, 2020, mshtakiwa na Regina walitoa Sh. 298,576,314 Benki ya GT kuzihamishia Benki ya CRDB wakionesha ni mishahara ya wafanyakazi wakati fedha hizo katika akaunti ya GT ziliwekwa na mshtakiwa ikiwa ni sehemu ya mkopo wa wafanyakazi hewa.

Inadaiwa mshtakiwa kwa kutumia fedha hizo za mkopo alinunua gari aina Ford Ranger lenye namba za usajili T 348 DVF kwa thamani ya Sh. 204,378,745.

Mshtakiwa alikubali maelezo hayo kuwa ni ya kweli na upande wa Jamhuri waliomba kutoa gari hilo kama kielelezo mahakamani na mahakama ilipokea.

Baada ya kusikiliza hoja hizo, Jaji Isaya alimtia hatiani mshtakiwa kwa kukiri makosa mawili ya kusababisha hasara na kutakatisha fedha.

Upande wa Jamhuri baada ya mshtakiwa kutiwa hatiani, uliomba mahakama itoe amri gari lenye namba za usajili T348 DVF aina ya Ford Ranger litaifishwe kuwa mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania.

Wakili wa Utetezi, Jeremiah Mtobesya aliomba mteja wake apunguziwe adhabu kwa kuwa ni mkosaji wa mara ya kwanza, ameipunguzia gharama mahakama ya kuita mashahidi, ana familia inamtegemea na ameshalipa Sh. milioni 100 kama sehemu yake ya mkataba.

"Mahakama imezingatia hoja za pande zote mbili, ninamhukumu mshtakiwa kulipa faini ya Sh. 500,000 au kwenda jela miaka mitano kwa shtaka la 180.

"Ninamhukumu mshtakiwa kulipa faini ya Sh. 500,000 au kwenda jela miaka mitano kwa shtaka la 181," alisema Jaji Isaya.

Jaji Isaya alitoa amri kwamba gari lenye namba ya usajili T348 DVF aina ya Ford Ranger linataifishwa kuwa mali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania.

# PSSSF YATWAA USHINDI WA KWANZA TUZO ZA NBAA ZA UANDAAJI BORA WA HESABU MWAKA UNAOISHIA 2023







Treasury manager wa PSSSF Bi Vones Koka akipokea Tuzo kwa niaba ya DG wa PSSSF







Wafanyakazi wa pamoja na DG wa PSSSF Wakifurahia tuzo hiyo mara baada ya kuwasilishwa rasmi PSSSF





HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### DELAP AFIKIRIWA JUVENTUS

KLABU ya Juventus inafikiria kumnunua Liam Delap wa Ipswich na wametuma maskauti kumtazama mshambuliaji huyo wa England mwenye umri wa miaka 21, ambaye pia anazivutia Chelsea na Manchester United. ***(Mirror)***

### ZIRKZEE PIA AWINDWA

JUVENTUS pia inatazamia kumsajili kwa mkopo mshambuliaji wa Manchester United kutoka Uholanzi, Joshua Zirkzee, 23. ***(Gazzetta dello Sport)***

### MUANI, NKUNKU KUPISHANA

KLABU ya Paris St-Germain inavutiwa na mshambuliaji wa Chelsea na Ufaransa, Christopher Nkunku, 27, na huenda wakamtoa mshambuliaji wa Ufaransa, Randal Kolo Muani,25, kwa kubadilishana naye. ***(TBR Football)***

### CHIESA ATAJWA NAPOLI

WINGA wa Liverpool, Federico Chiesa, 27, ni chaguo ambalo Napoli inafikiria ili kuchukua nafasi ya Khvicha Kvaratskhelia ikiwa mshambuliaji huyo wa Georgia hatatia saini mkataba mpya katika klabu hiyo ya Serie A. ***(Il Napolista)***

### BARRY KWA MKOPO

KLABU ya Aston Villa huenda ikamkumbuka Louie Barry, 21, kutoka kwa mkopo Stockport Januari na kumpeleka kwa mkopo katika klabu ya Championship, huku Sheffield Wednesday na Middlesbrough wakiongoza mbio za kumsaka mshambuliaji huyo wa England. ***(Star)***

### ERIKSEN BASI TENA UNITED

KLABU ya Manchester United haina uwezekano wa kumpa Christian Eriksen, 32, mkataba mpya, huku mkataba wa sasa wa kiungo huyo wa kati wa Denmark ukikamilika mwishoni mwa msimu. ***(Florian Plettenberg)***

### DORGU AWANIWA PALACE

CRYSTAL Palace ni miongoni mwa klabu nyingi za Ulaya zinazohitaji kumnunua beki wa pembeni wa Lecce raia wa Denmark, Patrick Dorgu. ***(CaughtOffside)***

### RASHFORD RUKSA KUSEPA

KLABU ya Manchester United imemruhusu mshambuliaji wa England, Marcus Rashford, 27, kuondoka. ***(Fichajes)***

### CRISTANTE AYEYUKA EVERTON

KLABU ya Everton haina uwezekano wa kukamilisha mpango wa kumnunua kiungo wa kati wa AS Roma, Bryan Cristante, 29, wakati wa dirisha la usajili la Januari. ***(Football Insider)***

### CEBALLOS KUREJESHWA REAL

KIUNGO wa kati wa Hispania, Dani Ceballos, 28, anaweza kuwa njiani kuondoka Real Madrid huku Real Betis wakiwa na nia ya kumrejesha mchezaji huyo wa zamani wa Arsenal katika klabu hiyo. ***(Fichajes)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ... YA



# ARTETA: MABAO 7 KIPINDI CHA KWANZA NI UKICHAA

**LONDON,** England

**Sikujua rekodi hiyo, lakini inakwambia jinsi ulivyokuwa ni wazimu, timu zote...**

MIKEL Arteta amekitaja kipindi cha kwanza cha ushindi wa Arsenal wa mabao 5-2 dhidi ya West Ham kuwa ni "cha kichaa" baada ya mabao yote saba kufungwa katika dakika 45 za kwanza za mchezo huo.

**Arsenal walitangulia kwa mabao 4-0 ndani ya dakika 36 kabla ya West Ham kufunga mawili, halafu Bukayo Saka akafunga mkwaju wa penalti katika muda wa lala salama za kipindi cha kwanza.**

Mchezo huo wa Jumamosi kwenye Uwanja wa London uliweka rekodi kwenye Ligi Kuu England kwa kufungwa mabao mengi zaidi kipindi cha kwanza (saba).

Ni mara ya nne tu katika historia kwa mabao saba kufungwa katika dakika 45 za kipindi cha kwanza mechi ya Ligi Kuu England - mara ya mwisho ni ushindi wa 4-3 wa Manchester United dhidi ya Reading Desemba 2012.

"Sikujua rekodi hiyo," alisema Arteta.

"Lakini inakuambia jinsi ulivyokuwa ni wazimu, jinsi timu zote mbili zilivyokuwa na ufanisi mbele ya lango. Ilikuwa ya kuvutia dakika 30 na mara moja unaweza kuona ni kiasi gani timu ilijitoa, madhumuni, uamuzi na ubora.

"Lakini baada ya hapo, tulikuwa na kipindi ambapo ubora wa mtu mmoja mmoja ulikuwa na jukumu kubwa.

"Unaweza kuhisi mabadiliko ya nguvu na unafikiri nini kinafuata? Ilikuwa nzuri kufunga mabao matano kwa sababu ni wazi kwamba ilituliza kila kitu na katika kipindi cha pili tunaweza kucheza mchezo tofauti sana ambao ulitufaa sana."

Arsenal walichukua uongozi baada ya dakika 10 kupitia kwa Gabriel Magalhaes aliyefunga kwa kichwa kabla ya Leandro Trossard kuongeza la pili.

Mkwaju wa penalti wa Martin Odegaard dakika ya 34 uliongeza faida yao na Kai Havertz akafunga dakika mbili baadaye huku baadhi ya mashabiki wa nyumbani wakielekea nje na Bukayo Saka akafunga la tano kwa mkwaju wa penalti.

Matokeo hayo yanamaanisha kuwa Arsenal walipaa juu Jumamosi hadi katika nafasi ya pili nyuma ya Liverpool ambao jana Jumapili walikuwa wakicheza na Manchester City kwenye Uwanja wa Anfield.



# KANE AZUA HOFU BAYERN

**DORTMUND,** Ujerumani

MSHAMBULIAJI wa Bayern Munich, Harry Kane yupo shakani kuwapo kwenye mechi yao ya Kombe la Ujerumani dhidi ya Mabingwa Bayer Leverkusen kesho Jumanne baada ya kupata jeraha katika sare ya bao 1-1 dhidi ya Borussia Dortmund katika mchezo wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, Jumamosi, kocha Vincent Kompany amesema.

Nahodha huyo wa England na mfungaji bora wa Bundesliga alitolewa baada ya dakika 33 wenyeji wakiwa mbele kwa bao 1-0.

Bayern walipoteza nafasi nyingi nzuri katika kipindi cha pili kabla ya Jamal Musiala kuokoa pointi moja kwa vinara wa ligi hiyo kwa bao la kichwa dakika ya 85.

"Hisia za Harry ni kwamba inaweza isiwe jambo zito sana," alisema Kompany akiwambia waandishi wa habari.

"Lakini itabidi tusubiri itabidi afanyiwe vipimo ndipo tutajua zaidi.

"Lakini ni wazi itakuwa ngumu kucheza Jumanne. Sijui wachezaji wengi ambao wanaweza kupona haraka," alisema Kompany.

Bayern, ambao kabla ya Jumamosi walikuwa wameshinda mechi zao saba za awali katika michuano yote bila kuruhusu bao hata moja, wanaikaribisha Leverkusen katika hatua ya 16 bora ya Kombe la Ujerumani kesho, Jumanne.

"Mabao ya Harry ni magumu sana, kuchukua nafasi yake ni ngumu," alisema kocha huyo.

"Huwezi kuchukua nafasi ya wachezaji wa ubora wake na mahali pengine, lakini wengine wanaweza kufanya hivyo pamoja."

# Flick alia na muunganiko Barca



**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona, Hansi Flick, anahisi kutokuwapo kwa muunganiko kati ya safu ya ulinzi na ushambuliaji kunaathiri timu yake baada ya mbio zao za LaLiga kutibuliwa kwa kufungwa mabao 2-1 na Las Palmas Jumamosi.

Sandro Ramirez na Fabio Silva walifunga katika vipindi tofauti kwa Las Palmas, huku Raphinha akiifungia Barca la kufutia machozi kwenye Uwanja wa Olympic na kuharibu sherehe zao za miaka 125 tangu kuanzishwa kwa klabu hiyo.

Barca sasa hawajashinda mechi ya ligi tangu Novemba 3 na wanaweza kung'olewa kileleni mwa jedwali kama Real Madrid ilishinda jana.

"Ninawaamini wachezaji," alisema Flick katika mkutano na waandishi wa habari alipoulizwa kuhusu kushuka kwa kiwango cha timu yake tangu kushinda mechi 11 za ufunguzi wa LaLiga.

"Tuna timu nzuri. Mechi kama za leo (juzi) haikuwa sawa. Nilipoanza hapa, niliwaambia wachezaji 'hakuna visingizio.' Lazima tuendelee kama timu.

"Unapocheza kama timu, au bora kuliko kama timu, na kila mtu analinda vizuri, ikiwa ni pamoja na kuunganishwa vizuri, tunaweza kucheza na kushinda dhidi ya kila timu.

"Lakini ikiwa sivyo, ikiwa wachezaji wengine wamekatishwa, basi si vizuri na lazima tuzungumze juu ya hilo."

Ulinzi mbovu haswa ulisababisha bao la pili la Las Palmas, lililofungwa na Silva baada ya bao la 14 la Raphinha katika kuirejesha Barca mchezoni, lakini Flick alisisitiza kuwa ni tatizo la timu.

"Unapoona jinsi mabao ya Las Palmas yalivyofungwa, tunafanya makosa, lakini haikuwa tu ya nne ya mwisho. Na tunapaswa kuzungumza juu ya hilo."

Kupoteza kwa Las Palmas kunakuja baada ya kutoka sare na Celta Vigo, wakati Barca walisalimu amri kwa mabao mawili, na kufungwa na Real Sociedad.

"Tunaweza kufanya hivyo. Tuna ubora. Leo (juzi) tulimiliki mpira kwa asilimia 70 na mashuti 27. Nilikosa ufanisi huo mbele ya lango kufunga mabao."

# Van Dijk akataa kuhusishwa na Madrid

**LIVERPOOL,** England

VIRGIL van Dijk amepuuzilia mbali mapendekezo ya uhamisho wa kwenda Real Madrid majira ya kiangazi lakini akakiri "hana la kusema" lilipokuja suala la kuongezwa kwa mkataba wake pale Liverpool.

Beki huyo wa Uholanzi, aliyetimiza umri wa miaka 33 Julai mwaka huu, anakaribia miezi sita ya mwisho ya mkataba wake wa sasa pale Anfield, lakini hatma ya uhakika haionekani.

Edu Aguirre wa El Chiringuito alipomuuliza Van Dijk kama atabakia Liverpool zaidi ya msimu wa joto, alijibu:

"Hawaniulizi hivyo, lakini sikiliza kwa sasa hakuna ninachoweza kusema. Kitu pekee ninachoweza kusema ni kuwa nimejikita kwenye mechi zinazokuja."

Mahojiano yaligeuka kuwa uwezekano wa kuhamia Madrid kwa Van Dijk, ambaye alikumbushwa kwamba Eder Militao na David Alaba wanapambana na majeraha.

Alipoulizwa tena kuhusu nafasi ya kujiunga na Madrid wakati mkataba wake wa Liverpool utakapomalizika, Van Dijk alijibu:

"Lini? Katika majira ya joto? Kama nilivyokwambia hapo awali, lengo kuu kwangu mechi inayofuata."



## HABARI MICHEZO

# OUMA AFUNGUKA SABABU ZA KUKUBALI KUJIUNGA SINGIDA BS

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA mpya Msaidizi wa Singida Black Stars, David Ouma, amezungumza kwa mara ya kwanza baada ya kuteuliwa kushika nafasi hiyo, akisema malengo makubwa na ushindani wanaouonesha wachezaji wa timu hiyo kwenye Ligi Kuu, ndiyo uliomfanya kukubali kutua kwenye kikosi hicho.

Akizungumza juzi baada ya kujiunga rasmi na kikosi hicho, Ouma, alisema alikuwa na ofa nyingi mkononi za klabu mbalimbali hapa nchini, lakini ameichagua timu hiyo kutokana na kuwa na malengo makubwa na ya ushindani, huku mwenyewe akiwa ni mshindani kamili.

"Malengo waliyokuwa nayo yamenipa matamanio makubwa ya kujiunga nao, kulikuwa na timu nyingi zilikuwa zikinihitaji, lakini nimeichagua Singida Big Stars, wana malengo makubwa, mimi napenda kushindana.

"Na walipokuja walikuja moja kwa moja na kuniambia nini wanataka na mimi nikawapa ya kwangu tukaelewana. Niwashukuru wachezaji, viongozi na mashabiki wa Singida Black Stars, nimekaribishwa vizuri, kilichobaki sasa ni kufanya kazi," alisema Ouma.

Kabla ya kujiunga na timu hiyo, Ouma raia wa Kenya, alikuwa na kikosi cha Coastal Union msimu uliopita, ambapo alikiwezesha kushika nafasi ya nne mwishoni mwa Ligi Kuu msimu uliopita na kucheza michuano ya kimataifa, Kombe la Shirikisho Afrika msimu huu.

**Hata hivyo, Coastal Union ilitolewa hatua za awali kwa kufungwa kwa jumla ya mabao 3-0 na Bravo do Maquis ya Msumbiji, iliyocheza na Simba Jumatano iliyopita kwenye michuano hiyo.**

Ilichapwa mabao 3-0 ugenini, kabla ya kutoa suluhu nyumbani, matokeo ambayo yalimfanya kuondoshwa kwenye timu hiyo, akiwa kocha wa kwanza kutimuliwa kwa timu za Ligi Kuu.

Singida Black Stars hivi karibuni iliwasimamisha makocha wake wawili, Patrick Aussems na Danis Kitambi kutokana na kile ambacho uongozi ulisema ni mwenendo usioridhisha wa timu hiyo.

Licha ya kusema imewasimamisha, lakini tayari klabu hiyo imemtangaza Ouma kama kocha msaidizi, huku pia kukiwa na tetesi za kocha wa zamani wa Yanga, Miguel Gamondi, kushika nafasi ya ukocha mkuu.

# JKT TANZANIA YATAMBA KUGAWA DOZI LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya ushindi wa bao 1-0 iliyoupata Ijumaa dhidi ya Fountain Gate, Ofisa Habari wa JKT Tanzania, Masau Bwire, ametamba kuwa timu hiyo imerejea rasmi Ligi Kuu kwa ajili ya kazi moja tu ya kugawa dozi kwa kila timu itakayokutana nayo.

Akizungumza juzi akiwa Babati mkoani Manyara, Masau alisema wachezaji wao walikuwa 'wamemisi' mikiki ya ligi, na sasa wamerejea tena kwa nguvu na ari mpya, huku wakipata ushindi wa pili mfululizo.

Timu hiyo ilikuwa inacheza mchezo wa pili, baada ya kukaa nje kwa siku 29 kutokana na wachezaji wake kupata ajali baada ya basi la timu hiyo kupinduka lilipokuwa likitoka jijini Dodoma, kucheza mchezo wa Ligi Kuu Tanzania bara, dhidi ya Dodoma Jiji, kwenye Uwanja wa Jamhuri, Oktoba 26, mwaka huu, na kujeruhi wachezaji 11.

Baada ya ajali hiyo, Bodi ya Ligi iliahirisha michezo kadhaa ya timu hiyo, ambapo ilirejea dimbani, Novemba 24, mwaka huu, ilipocheza dhidi ya Prisons na kushinda bao 1-0 kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, ikishinda mchezo wa pili mfululizo Ijumaa iliyopita dhidi ya Fountain Gate, ikiwa ugenini, Uwanja wa Tanzania Kwaraa, Babati, Manyara.

"Tumerejea kwenye Ligi Kuu, hii ni mechi ya pili mfululizo tunashinda tangu kuanza tena mchezo yetu, nizitahadharishe tu timu zilizobaki kuwa JKT Tanzania tumerejea kwa ajili ya kutoa dozi, tumeanza na Prisons, halafu Fountain Gate, bado wengine wajiandae," alitamba.

JKT Tanzania inatarajia kucheza mechi yake ijayo dhidi ya Pamba Jiji, Desemba 11, mwaka huu, Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Dar es Salaam.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Ahmad Ally, aliwashukuru wachezaji wake, akisema pamoja na misukosuko waliyoipata, lakini bado wameendelea kuwa watulivu na wasikivu wakati wa mafundisho yake, kwani wanachokitoa uwanjani ndicho alichokuwa akiwafundisha kwenye uwanja wa mazoezi.

Timu hiyo ipo kwenye nafasi ya nane ya msimamo wa Ligi Kuu, ikiwa na pointi 16, ikicheza mechi 11 hadi sasa.

## Simba waapa kwenda kupambania 3 Algeria

INATOKA UKURASA 24

ushindi siku zote si zawadi bali ni kushindana, akisema huwezi kwenda uwanjani ukatarajia kushinda kama hujaandaa vizuri kikosi kwenye uwanja wa mazoezi.

"Tunaitengeneza timu ili kwenda kushinda mechi, malengo ya klabu ni kufika hatua ya robo fainali, lakini hauwezi kufika kama hushindi mchezo. Tunakwenda kucheza na CS Constantine, nadhani inaweza kuwa ni timu ngumu zaidi kwenye kundi hili, inacheza vizuri, ina kikosi kizuri, lakini tutakwenda kupambana," alisema Fadlu.



Kiungo wa Yanga, Clatous Chama, akiitoka safu ya ulinzi ya Namungo FC, kabla ya kugawa pasi ya upendo kwa Pacome Zouzoua, iliyozaa bao la pili kwa timu hiyo, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi juzi. Yanga ilishinda mabao 2-0. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Ramovic akoshwa kiwango Chama*

INATOKA UKURASA 24

"Nawapongeza pia wapinzani wetu ni timu ngumu, walikuwa wanakaa nyuma wengi na wakishambulia mbele wakiwa watu wanne, ilikuwa ngumu kukabiliana nao," alisema.

Hakusita kumpa maua yake, Chama, akisema ni mchezaji maalum, kwani kuingia kwake kuliibadilisha kabisa timu na yeye ndiye aliyetoa 'asisti' iliyotengeneza mabao yote mawili kwenye mchezo huo.

Chama ameingia na kuibadilisha timu, ametoa 'asisti' mabao yote mawili, ni mchezaji mzuri sana, hivyo wachezaji wengine wanapaswa kuboresha viwango vyao, ingawa najua kikosi kina wachezaji wenye uwezo wa juu," alisema kocha huyo.

Yalikuwa ni mabao ya Kennedy Musonda na Pacome Zouzoua, yaliyoifanya Yanga kufikisha pointi 27, sawa na Azam FC, zote zikiwa na mabao 16 zikiruhusu manne, lakini 'Wanajangwani' hao bado wako nafasi ya tatu kwa alfabeti, ingawa imecheza mechi 11, huku 'Wanalambalamba' wakiwa na michezo 12, jana wakitarajia kucheza dhidi ya Dodoma Jiji.

Kocha Mkuu wa Namungo, Juma Mgunda, ambayo timu yake imepoteza mchezo wa tatu mfululizo, amesema ubora wa wachezaji wa Yanga ndiyo ulioamua mechi.

"Nimekubali matokeo, si mazuri, lakini ni ya mpira, niseme tu ubora wa wachezaji wa Yanga umeamua mechi, naendelea kuiboresha timu, siku za mbele itakaa vizuri," alisema Mgunda.

Kipigo hicho kinaifanya Namungo kukaa nafasi ya 14, ikicheza mechi 12 na kujikusanyia pointi tisa tu.

# Michezo

Jumatatu Desemba 2, 2024

Nipashe




‘Mabao 7 kipindi cha kwanza ni ukichaa’ UKURASA 21

# Simba waapa kupambania tatu Algeria

## ●●● Kuifuata CS Constantine Jumatano, Fadlu afunguka huku wachezaji wakisema ni...

Na Adam Fungamwango

WACHEZAJI wa Simba, wamesema watakwenda kupigana kufa kupona ili kupata ushindi au hata sare kwenye mchezo wa pili wa Kombe la Shirikisho, hatua ya makundi dhidi ya CS Constantine ya Algeria, huku Kocha Mkuu wa timu hiyo, Fadlu Davids akisisitiza ni ushindi tu.

**Kikosi cha Simba kinatarajia kuondoka keshokutwa, Jumatano kwenda kwenye mji wa Constantine kucheza mechi hiyo ya Kundi A, dhidi ya timu hiyo utakaopigwa, Jumapili saa 1:00 usiku katika Uwanja wa Mohamed Hamlaoui.**

Akizungumza kwa niaba ya wenzake, mchezaji mkongwe wa timu hiyo, Mzamiru Yassin, alisema wao kama wachezaji wako kwenye mazoezi makali kwa ajili ya maandalizi kwani wanatambua hautakuwa mchezo rahisi kama wengi wanavyodhani, lakini dhamira yao ni kwenda kusaka pointi katika mchezo huo.

“Mechi ni ngumu, si nyepesi kama watu wanavyofikiria, sisi wengine ni wazoefu kwenye michuano hii, tunajua hilo, kinachotuaminisha hivyo ni kwamba mpinzani wetu tunaekwenda kucheza naye ametoka kushinda ugenini, akiifunga timu kubwa kama CS Sfaxien ya Tunisia ambayo kwenye kundi letu ndiyo ina historia nzuri ya michuano hii kuliko timu yoyote.

“Kama hao jamaa Watunisia wamefungwa kwao, ina maana si timu ya kubeza, ndiyo maana tumekomaa kwenye mazoezi,” alisema mchezaji huyo aliyejiunga na timu hiyo mwaka 2016, akitokea Mtibwa Sugar.

CS Sfaxien, imetwaa Kombe la Shirikisho Afrika mara tatu, mwaka 2007, 2008 na 2013.

Alisema wachezaji wa Simba wanatambua kuwa wapinzani wao watataka kushinda mchezo huo ili waongeze matumaini ya kusonga mbele baada ya kushinda ugenini, hivyo hawatokubali kuona hilo likitokea.

“Ni mechi ambayo wapinzani wetu wataichukulia umuhimu sana kwani wameshashinda ugenini, watataka kushinda kwao ili wawe kwenye nafasi nzuri ya kufuzu makundi, wachezaji tunajua hilo, ndiyo maana tumejiandaa kwenda kuchukua pointi tatu, ikishindikana moja kwani tayari tumeshachukua tatu nyumbani dhidi ya Bravo do Maquis, nao pia watakuja nyumbani,”, alisema mchezaji huyo anayecheza nafasi ya kiungo mkabaji.

Alilisifia benchi la ufundi la timu hiyo, likiongozwa na Fadlu Davids kuwa linafanya kazi kubwa na akikiri kwa miaka ya karibuni hajaona benchi bora kama hilo.

“Nafasi ya kusonga mbele hatua ya robo fainali tunayo, ila haitoki mdomoni, bali kwa jitihada, lakini naamini tutapita kwani safari hii tuna benchi la ufundi zuri sana,” alisema.

Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu, amesema



INAENDELEA UKURASA 23



Kiungo wa Simba, Yusuph Kagoma, akiwa mazoezini katika Uwanja wa Mo Simba Arena kujiandaa na mechi ijayo ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya CS Constantine ya Algeria Jumapili wiki hii nchini humo. **PICHA: SIMBA**

# Ramovic akoshwa kiwango Chama

Na Adam Fungamwango

KOCHA Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic, amesifu kiwango cha kiungo mshambuliaji, Clatous Chama, akisema ni cha hali ya juu na ndiye aliyebadilisha mchezo kiasi cha kushinda mabao 2-0 katika mechi ya juzi dhidi ya Namungo iliyopigwa Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi.

Kocha huyo pia amesema ameridhishwa na kiwango cha wachezaji wake akisema vinapanda taratibu ingawa bado havijawa kwa asilimia zote, hasa upande wa pumzi na utimamu wa mwili.

Yanga imepata ushindi huo kwa mara ya kwanza, baada ya kupoteza michezo mitatu mfululizo, miwili ya Ligi Kuu Bara, ikifungwa bao 1-0 dhidi ya Azam FC, Novemba 2 na mabao 3-1, Novemba 7, mwaka huu na kisha kuangukia pua kwa kichapo cha mabao 2-0 dhidi ya Al Hilal ya Sudan kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

“Angalau leo nimeridhishwa na kiwango cha wachezaji wangu, katika mchezo wa leo nimeona wameanza kukaa sawa. Najua tumepata pointi tatu, lakini bado tunatakiwa kupandisha tena viwango vyetu juu na hasa upande wa pumzi na utimamu wa mwili, si rahisi lakini kidogo kidogo tutakaa sawa, kuna vitu vingine vya kufanya kama kocha, muhimu tumeshinda mchezo huu, ilikuwa muhimu sana kwetu kwanza kushinda kuliko kitu kingine,” alisema kocha huyo ambaye ni mchezo wake wa kwanza kuiongoza Yanga kwenye Ligi Kuu, lakini wa pili kwa michezo yote.

Kocha huyo raia wa Ujerumani aliwapongeza Namungo akisema ni timu nzuri na imewapa wakati mgumu.

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >